

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

مَا يَفْعَلُ اللّٰهُ بِعَذَابِكُمْ اِنْ شَكَرْتُمْ وَ
اٰمَنْتُمْ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ شَاكِرًا عَلِيْمًا ﴿١٤٧﴾

147. Mwenyezi Mungu hakuadhibuni kama mtashukuru na mtaamini. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kupokea shukurani(na)ndiye Mwenye kujua.

لَا يُحِبُّ اللّٰهُ الْجَهْرَ بِالسُّوْٓءِ مِنَ الْقَوْلِ اِلَّا
مَنْ ظُلِمَ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ سَمِيْعًا عَلِيْمًا ﴿١٤٨﴾

148. Mwenyezi Mungu hapendi kutoa maneno ya kutangaza ubaya (wa watu) ila kwa yule mwenye kudhulumiwa; na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye (na) ajuaye.

اِنْ تُبْدُوْا خَيْرًا اَوْ تُخْفُوْهُ اَوْ تَعْفُوْا عَنْ سُوْٓءٍ فَاِنَّ
اللّٰهَ كَانَ عَفُوًّا قَدِيْرًا ﴿١٤٩﴾

149. Mkidhihirisha wema au mkiuficha au mkiyasamehe maovu (ndiyo ndivyo) kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe (juu ya kuwa) Muweza.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَكْفُرُوْنَ بِاللّٰهِ وَ رُسُلِهٖ وَ يُرِيْدُوْنَ
اَنْ يُّفَرِّقُوْا بَيْنَ اللّٰهِ وَرُسُلِهٖ وَيَقُوْلُوْنَ نُؤْمِنُ
بِبَعْضٍ وَّنَكْفُرُ بِبَعْضٍ ۙ وَّيُرِيْدُوْنَ اَنْ
يَّتَّخِذُوْا بَيْنَ ذٰلِكَ سَبِيْلًا ﴿١٥٠﴾

150. Hakika wale wanaomkanusha Mwenyezi Mungu na Mitume yake, na wanataka kutenga baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume yake, kwa kusema: "Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa," na wanataka kushika njia iliyo kati kati ya haya (si ya Kiislamu khasa wala ya Kikafiri)

اُولٰٓئِكَ هُمُ الْكٰفِرُوْنَ حَقًّا ۚ وَاَعْتَدْنَا لِلْكٰفِرِيْنَ
عَذَابًا مُّهِيْنًا ﴿١٥١﴾

151. Hao ndio makafiri kweli. Na tumewaandalia makafiri adhabu idhalilishayo.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖ وَلَمْ يُفَرِّقُوْا بَيْنَ اَحَدٍ
مِّنْهُمْ اُولٰٓئِكَ سَوْفَ يُؤْتِيْهِمْ اُجُوْرَهُمْ ؕ
وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿١٥٢﴾

152. Na waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume yake wala wasimfarikishe yo yote katika wao (bali wamewaamini wote), hao atawapa ujira wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

---

katika Sura 4:70." Haya tumekwisha kuyajibu katika Aya ya 7 ya *Al Fatiha*.

148. Ndiyo hivi hapendi Mwenyezi Mungu watu kutaja maovu ya wengineo ila mwenye kudhulumiwa anapewa ruhusa kufikisha kwa hakimu maovu aliyofanyiwa ili amtozee haki yake. Lakini bure tu hivi kutangaza ubaya wa watu hapana ruhusa. Ni katika maasiya makubwa.

150. Madamu Mwenyezi Mungu amemkiri kuwa ni Mtume Wake na wewe ukakataa kumwamini, kama Mayahudi wanavyomkataa Nabii Isa, na Manasara—pamoja na Mayahudi—wanavyomkataa Nabii Muhammad; basi inakuwa ukafiri. Waislamu wanawakiri Mitume wa haki wote waliokuja *kabla* ya Nabii Muhammad.

Basi Waislamu wanawakubali Wajumbe hao wa Mwenyezi Mungu wote kama alivyobainisha Mwenyewe Mwenyezi Mungu katika Qurani. Na wanawakataa wale aliowakataa Mwenyezi Mungu katika Qurani kuwa hao si mitume wake. Nao ni wale wanaodai kuwa wamepewa Utume *baada* ya Nabii Muhammad.

Anayewaamini hao wanaojidai kuwa wamepata utume baada ya Nabii Muhammad—kama huyo Mirzai na Bahai—basi hao wanaojidai hivyo ni makafiri na wenye kuwakiria kwa hayo ni makafiri nao pia.

Basi natutahadhari madanganyo ya Makadiyani (Mirzai) na wenziwao. Huo wao ni uwongo mtupu, na wanasingizia tu hivyo vitabu wanavyovitaja na hao mashekhe wanaowadhukuru.

Katika Aya waliyoifanya ni ya 151 wametia maneno ya Ibni Kathir ili kudhanisha watu kuwa Ibni Kathir anamkubalishia Utume anayedai kupewa Utume baada ya Nabii Muhammad. Na wanajua wao — na kila Mwislamu — kuwa Ibni Kathir, ni kama Waislamu wengine, wanakataza kuwakataa Mitume wa haki waliokuwa KABLA ya Nabii Muhammad, kama Qurani yote inavyosema "MINQABLIKA" (Waliopewa Utume kabla ya Nabii Muhammad). Na tumekwisha kuyataja haya katika Aya ya 4 ya *Suratul Baqarah*. Ibni Kathir amekufa katika mwaka 700; miaka 600 kabla hakuzuka mtu wao mdai Utume.

153. Mayahudi walimwambia Mtume kuwa hawatamwamini mpaka wamwone anapaa mbinguni mikono mitupu na anarejea na Kitabu mkononi kilichoandikwa shahada ya Mwenyezi Mungu kuwa kweli Nabii Muhammad ni Mtume Wake.

يَسْـَٔلُكَ أَهْلُ الْكِتٰبِ أَنْ تُنَزِّلَ عَلَيْهِمْ كِتٰبًا مِّنَ السَّمَآءِ فَقَدْ سَأَلُوا مُوسٰٓى أَكْبَرَ مِنْ ذٰلِكَ فَقَالُوٓا أَرِنَا اللّٰهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْهُمُ الصّٰعِقَةُ بِظُلْمِهِمْ ۚ ثُمَّ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ مِنْ بَعْدِ مَا جَآءَتْهُمُ الْبَيِّنٰتُ فَعَفَوْنَا عَنْ ذٰلِكَ ۚ وَءَاتَيْنَا مُوسٰى سُلْطٰنًا مُّبِينًا ﴿١٥٣﴾

153. Watu waliopewa Kitabu (Mayahudi) wanakutaka uwateremshie Kitabu kutoka mbinguni. Na kwa hakika walimtaka Musa makubwa kuliko haya; wakasema: "Tuonyeshe Mungu wazi wazi." Ukawashika moto wa radi (uliowatoa roho zao) kwa sababu ya ukafiri wao. (Kisha Mwenyezi Mungu akawapa uhai mara ya pili). Kisha wakamfanya ndama (kuwa mungu) baada ya kuwafikia hoja (zote) zilizo wazi; lakini tukasamehe hayo na tukampa Musa hoja zilizo dhahiri (juu yao).

وَرَفَعْنَا فَوْقَهُمُ الطُّوْرَ بِمِيْثَاقِهِمْ وَقُلْنَا لَهُمُ ادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا وَّقُلْنَا لَهُمْ لَا تَعْدُوْا فِي السَّبْتِ وَأَخَذْنَا مِنْهُمْ مِّيْثَاقًا غَلِيْظًا ﴿١٥٤﴾

154. Na tukaunyanyua mlima juu yao (hao Mayahudi) kwa kufanya agano nao (la kufuata Taurat). Na tuliwaambia: "Liingieni lango (la nchi ya Shamu) hali ya kuinama (kama mnarukuu)"; (wakapinga). Na (pia) tukawaambia: "Msiruke mipaka kwa (kuvunja taadhima ya) Jumaamosi." Na tukachukua kwao ahadi iliyo madhubuti (kwa mambo haya na mengineyo; wala wasitimize).

فَبِمَا نَقْضِهِمْ مِّيْثَاقَهُمْ وَكُفْرِهِمْ بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَقَتْلِهِمُ الْأَنْۢبِيَآءَ بِغَيْرِ حَقٍّ وَّقَوْلِهِمْ قُلُوْبُنَا

155. Basi (tuliwaadhibu) kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi zao, na kuzikataa kwao hoja za Mwenyezi Mungu, na kuua kwao Manabii bila ya haki, na kwa kusema kwao (kumwambia Nabii

---

Basi Mwenyezi Mungu ndiyo anasema kuwa si ajabu hao Mayahudi kuleta upinzani namna huo: Wao walimfanyia upinzani Nabii Musa wakamwambia kuwa hawatamwamini kuwa yeye ni Mtume mpaka awaonyeshe Mwenyezi Mungu, wamwone uso na macho. Na walipokosa hayo walimchukua ndama (mtoto wa ng'ombe) wakamfanya ndiye mungu wakamwabudu.

154-156. Anaendelea Mwenyezi Mungu kutaja mabaya yao, mengine kama vile kuwa:—

(a) Walikataa kufuata amri za Taurati: Mwenyezi Mungu akaling'oa jabali likasimama juu ya vichwa vyao, wakaambiwa kama hawatakubali kuchukua ahadi ya kuifuata hiyo Taurati litawasagasaga jabali hilo.

(b) Walipinga kuingia lango la nchi ya Shamu kwa namna hiyo waliyoambiwa. Wakaingia wanavyotaka wao. Shamu ni nchi Mwenyezi Mungu aliyowapa waingie wakae baada ya kutoka Misri. Wala wasiishukuru neema hii kwa kufuata alivyowambia Mwenyezi Mungu.

(c) Na baada ya kutua katika hiyo miji na vijiji vya Shamu waliambiwa waiadhimishe siku ya Jumaamosi kwa kuifanya ni siku ya ibada tu, si siku ya kufanya kazi. Wakatiatia hila zao mpaka ikawa ni siku ya kazi.

(d) Baadhi ya Mitume yao walipowafanyia ukali juu ya haya na mengineyo waliwaua!

(e) Na Nabii Muhammad alipowabainishia dalili zilizomo vitabuni mwao zinazoonyesha dhahiri Utume wake walijitia pambani wakawa wanamwambia 'Nyoyo zetu zimefumbwa, hazifahamu lo lote katika hayo unayoyasema.'

(f) Na Nabii Isa alipowabainishia Utume wake na Miujiza ile iliyotokea katika kuzaliwa kwake walimkataa kuwa Mtume na wakasema kuwa Bibi Maryamu kashika mimba yake kwa kuzini. Nao wanajua kuwa ni uwongo, lakini basi tu wanajitia pambani.

(g) Wakafanya hila ili wamuue huyu Nabii Isa. Lakini Mwenyezi Mungu aliipindua ile hila yao—akamtia kidogo mshabaha wa Nabii Isa yule mkubwa wa hila ya kutaka kumwua Nabii Isa. Na kwa fazaa wakamwua huyo wenziwao na wakamsulubu; na Nabii Isa akarufaishwa na Mwenyezi Mungu.

Baadaye wale wakubwa walitambua haya yaliyotokea lakini walijitia pambani vile vile wakawa wanajigamba kuwa, "Tumemuua huyo Masihi, Mtume wa Mungu; (nini kitakuwa)."

Na mabaya yao mengine yanafahamika dhahiri katika Aya hizi.

157. Wametia Ukafiri wao hapa katika hii Aya walioifanya kuwa ya 158 wakalifasiri uwongo tamko la "*Wamaasalabuuhu.*" Tafsiri yake kama ilivyo katika vitabu vya tafsiri vyote, na ilivyo katika vitabu vya kufasiri maneno magumu ya Qurani kama hiyo *Al Mufradat* na ilivyo katika Makamusi ya lugha ya Kiarabu yaliyotungwa

غُلْفٌ ۚ بَل طَبَعَ اللَّهُ عَلَيْهَا بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٥٥﴾

Muhammad): "Nyoyo zetu zimefumbwa (haziwezi kuingia kitu katika hayo unayoyasema"); (wala hazikufumbwa), bali Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri kwa kufuru zao, kwa hivyo hawaamini ila kidogo tu.

وَّبِكُفْرِهِمْ وَقَوْلِهِمْ عَلَىٰ مَرْيَمَ بُهْتَانًا عَظِيمًا ﴿١٥٦﴾

156. Na kwa sababu ya kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa (kuwa kamzaa Nabii Isa kwa kuzini)

وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ ۖ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَٰكِن شُبِّهَ لَهُمْ ۚ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ مِّنْهُ ۚ مَا لَهُم بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتِّبَاعَ الظَّنِّ ۚ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا ﴿١٥٧﴾

157. Na kwa (ajili ya) kusema kwao: "Sisi tumemuua Masihi Isa, mwana wa Maryamu Mtume wa Mungu," hali hawakumwua wala hawakumsulubu, bali walibabaishiwa (mtu mwengine wakamdhani Nabii Isa). Na kwa hakika wale waliokhitalifiana katika (hakika) hiyo (ya kumwua Nabii Isa) wamo katika shaka nalo (jambo hilo la kusema kauawa). Wao (kabisa) hawana yakini juu ya (jambo) hili (la kuwa kweli wamemwua Nabii Isa), isipokuwa wanafuata dhana tu. Na kwa yakini hawakumwua

بَل رَّفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٥٨﴾

158. Bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

وَإِن مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ إِلَّا

159. Na hakuna yo yote katika watu waliopewa Kitabu (Mayahudi na Manasara) ila humwamini

---

na Waislamu kama *Al Qamus*, na yaliyotungwa na wasiokuwa Waislamu kama *Al Munjid*. Vitabu vyote hivyo vinafasiri *Salaba* = Kumtundika au kumgongomelea katika msalaba, akifa humo au kawahi kuteremshwa kabla ya kufa. Katika hiyo *Al Mufradat* imeandikwa hivi: *"Assalbu = Taalyqul Insani lilqatli"* = (Kumtundika mtu kwa ajili auawe). Akasema tena; *"Shaddu Sulbihy Alaa Khashab"* = (Kuufunga mgongo wake katika ubao). Hakusema "Kumwua juu ya msalaba"

Na wafasiri wote wamesema hivi. Na wao wasijali wasibali wakaandika uwongo huu: "Neno hili maana yake ni kuua kwa kupigilia au kufunga mtini." Kwa hivi wakafasiri "hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani." Wamemkubalishia Nabii Isa kusulubiwa ila hakufa tu juu ya msalaba. Na hii ni kinyume ya Itikadi ya Waislamu. Waislamu wanasema — KAMA ALIVYOSEMA Mwenyezi Mungu hapa kuwa hawakumuua bali hata kumsulubu pia hawakuweza; hawakupatanafasi ya kumwua wala nafasi ya kumsulubu tu kisha akateremshwa; pia fursa hii hawakuipata, ilivyokuwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe kamhifadhi Mtume Wake. Wao wanamkanusha Mungu wanamwambia: "Kasulubiwa—wewe Mungu huna habari! Wao wanayajua kuliko Mungu! Pana ukafiri zaidi kuliko huu wa kujiona wao wanajua hakika kuliko Mwenyezi Mungu? Na tumeyasema haya katika Aya ya 54 ya *Aali Imrani*. Basi hana ruhusa Islamu kuitakidi hii itikadi ya kikafiri ya kuwa Nabii Isa alisulibiwa. Tusiharibiwe dini yetu na Wakristo na hawa nao. Na wanajidai kutaja Kamusi la Lane na Akrab. Uwongo; hamna humo wasemayo wao. Kudanganya tu huko.

Na ile *"Walaakin Shubbihalahum"* (Wameshabihishiwa mtu mwengine), wameikoroga wakasema: "bali alifananishwa kwao (kama maiti)". Liko wapi hilo tamko la maiti hapo? Wanataka kupoteza tu.

158. Mpinduo wao wa Aya hii walioifanya ya 159 tumekwisha kuubainisha katika Aya ya 56 ya *Aali Imrani*.

159. Katika Aya hii walioifanya ni ya 160 wamejidai kuandika *"Kabla ya kifo chake"*, yaani kabla ya kifo chao (Wakristo na Mayahudi, alivyosimulia Ubayy (Jarir, Jalada 1, uk. 13). Si mradi wake kusema *kabla ya kifo chake* ni kabla ya kifo cha Nabii Isa. . ." Wamefanya hivi kusudi kukimbia itikadi ya kuwa Nabii Isa atarejea, na hali ya kuwa ndivyo Mtume alivyosema, ikasihi kauli yake hii katika Hadithi za Al Bukhary na nyinginezo. Na hivyo kumtaja Ubayy na Ibni Jarir ni katika hayo madanganyo yao ili idhaniwe kuwa hiyo tu ndiyo tafsiri iliyo

(Nabii Isa kwa hakika yake) kabla ya kifo cha kila mmoja katika hao. (Lakini hakuna faida kumwamini huko wakati huo). Naye (Masihi) siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

لَيُؤْمِنَنَّ بِهٖ قَبْلَ مَوْتِهٖ ۚ وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ يَكُوْنُ عَلَيْهِمْ شَهِيْدًا ﴿١٥٩﴾

160. Basi kwa dhulma yao hao Mayahudi tuliwaharimishia vitu vizuri walivyohalalishiwa, na (vile vile) kwa sababu ya kuzuilia kwao watu wengi na njia ya Mwenyezi Mungu

فَبِظُلْمٍ مِّنَ الَّذِيْنَ هَادُوْا حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ طَيِّبٰتٍ اُحِلَّتْ لَهُمْ وَبِصَدِّهِمْ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ كَثِيْرًا ﴿١٦٠﴾

161. Na kwa (sababu ya) kula kwao riba, na hali wamekatazwa wasiile, na (kadhalika) kwa kula kwao mali za watu kwa batili. Basi tumewaandalia makafiri—nao ndio wao—adhabu iumizayo.

وَّاَخْذِهِمُ الرِّبٰوا وَقَدْ نُهُوْا عَنْهُ وَاَكْلِهِمْ اَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ ۭ وَاَعْتَدْنَا لِلْكٰفِرِيْنَ مِنْهُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿١٦١﴾

162. Lakini wale waliozama barabara katika ilimu miongoni mwao (hawa waliopewa Kitabu), na Waislamu; (ambao wote hao) wanaamini yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako, na (wale) wanaodumisha Sala na wanaotoa Zaka na wanaomwamini Mwenyezi Mungu (wakafuata amri Zake wakajiepusha na makatazo Yake) na (wanaamini) siku ya mwisho (wakaitengenezea amali njema). Hao tutawapa malipo makubwa.

لٰكِنِ الرّٰسِخُوْنَ فِي الْعِلْمِ مِنْهُمْ وَالْمُؤْمِنُوْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِمَآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ وَمَآ اُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَالْمُقِيْمِيْنَ الصَّلٰوةَ وَالْمُؤْتُوْنَ الزَّكٰوةَ وَالْمُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ۭ اُولٰۗىِٕكَ سَنُؤْتِيْهِمْ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿١٦٢﴾

163. Tumekuletea wahyi kama tulivyowapelekea Nuhu na Manabii (wengine) baada yake. Na (kama) tulivyowapelekea Ibrahimu na Ismaili na Is-haqa na Yaaqubu na kizazi (chake). Na (kama tulivyowapelekea) Isa na Ayyubu na Yunusi na Haruni na Suleimani; na Daudi tukampa Zaburi.

اِنَّآ اَوْحَيْنَآ اِلَيْكَ كَمَآ اَوْحَيْنَآ اِلٰى نُوْحٍ وَّالنَّبِيّٖنَ مِنْۢ بَعْدِهٖ ۚ وَاَوْحَيْنَآ اِلٰٓى اِبْرٰهِيْمَ وَاِسْمٰعِيْلَ وَاِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ وَالْاَسْبَاطِ وَعِيْسٰى وَاَيُّوْبَ وَيُوْنُسَ وَهٰرُوْنَ وَسُلَيْمٰنَ ۚ وَاٰتَيْنَا دَاوٗدَ زَبُوْرًا ﴿١٦٣﴾

164. Na (tuliwapelekea wahyi) Mitume tuliokuhadithia (habari zao) zamani na Mitume ambao hatukukuhadithia (habari zao). Na Mwenyezi Mungu akamsemeza Musa.

وَرُسُلًا قَدْ قَصَصْنٰهُمْ عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ وَرُسُلًا لَّمْ نَقْصُصْهُمْ عَلَيْكَ ۭ وَكَلَّمَ اللّٰهُ مُوْسٰى تَكْلِيْمًا ﴿١٦٤﴾

---

sahihi; na hali ya kuwa zote mbili hizo ni tafsiri sahihi. Ikiwa hiyo waliyoitaja wao imetegemewa na huyo Sahaba Bwana Ubayy kama alivyobainisha Mufassir Ibni Jarir, basi huyo Ibni Jarir kabainisha papo hapo Masahaba waliosema hiyo tafsiri nyingine—kama Bwana Abdalla bin Abbas na Bwana Abu Hureyra—na Maimamu wengine walioitaja hiyo tafsiri ya pili, kama Abu Malik, Al Hasanul Bisry, Qatada, Ibni Zaid na Attabary, kama alivyoyabainisha haya mwenye *Ruuhul Maany* katika sahifa 12 ya Juzuu ya 6; na wengineo pia na wakawataja zaidi kuliko hawa. Na wanajua hawa lakini basi tu; shauku ya kuwapoteza Waislamu imewashika.

162. Anataja hapa Mwenyezi Mungu kuwa Mayahudi wazuri walisilimu. Nayo ndio kweli; walisilimu zama za Mtume, wakawa wanavyuoni wakubwa kabisa, na baadaye vile vile.

163. Yanatajwa baadhi ya majina ya Mitume.

164. Inaonyesha kuwa kuna chungu ya Mitume ambao hayakutajwa majina yao katika Qurani. Basi zile Hadithi zinazotaja idadi ya Mitume wakubwa na wadogo si sahihi—dhaifu.

166. Mwenyezi Mungu anamtia nguvu Mtume wake na kumwambia kuwa yeye mwenyewe anamshuhudia

رُسُلًا مُّبَشِّرِيْنَ وَمُنْذِرِيْنَ لِئَلَّا يَكُوْنَ لِلنَّاسِ عَلَى اللّٰهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۚ وَكَانَ اللّٰهُ عَزِيْزًا حَكِيْمًا ﴿١٦٥﴾

165. (Hao ni) Mitume waliotoa khabari nzuri (kwa watu wema), wakawaonya (wabaya), ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya (kuletwa hawa) Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

لٰكِنِ اللّٰهُ يَشْهَدُ بِمَآ اَنْزَلَ اِلَيْكَ اَنْزَلَهٗ بِعِلْمِهٖ ۚ وَالْمَلٰٓئِكَةُ يَشْهَدُوْنَ ۚ وَكَفٰى بِاللّٰهِ شَهِيْدًا ﴿١٦٦﴾

166. Lakini Mwenyezi Mungu anayashuhudia aliyokuteremshia (kuwa ni haki). Ameyateremsha kwa ilimu yake. Na Malaika (pia) wanashuhudia. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ قَدْ ضَلُّوْا ضَلٰلًا بَعِيْدًا ﴿١٦٧﴾

167. Hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu bila shaka wamepotea upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki).

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَظَلَمُوْا لَمْ يَكُنِ اللّٰهُ لِيَغْفِرَ لَهُمْ وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ طَرِيْقًا ﴿١٦٨﴾

168. Hakika wale waliokufuru na kudhulumu haitakuwa kwa Mwenyezi Mungu kuwasamehe wala kuwaongoza njia

اِلَّا طَرِيْقَ جَهَنَّمَ خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اَبَدًا ۚ وَكَانَ ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرًا ﴿١٦٩﴾

169. Isipokuwa njia ya Jahannamu. Humo watakaa daima milele. Na hayo ni rahisi kwa Mwenyezi Mungu.

يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَكُمُ الرَّسُوْلُ بِالْحَقِّ مِنْ رَّبِّكُمْ فَاٰمِنُوْا خَيْرًا لَّكُمْ ۚ وَاِنْ تَكْفُرُوْا فَاِنَّ لِلّٰهِ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ وَكَانَ اللّٰهُ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿١٧٠﴾

170. Enyi watu! Mtume amekufikieni kwa haki kutoka kwa Mola wenu. Basi aminini; itakuwa bora kwenu. Na kama mtakataa basi ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi(na) Mwenye hikima.

يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ لَا تَغْلُوْا فِىْ دِيْنِكُمْ وَلَا تَقُوْلُوْا عَلَى اللّٰهِ اِلَّا الْحَقَّ ۚ اِنَّمَا الْمَسِيْحُ عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ رَسُوْلُ اللّٰهِ وَكَلِمَتُهٗ ۚ اَلْقٰىهَآ اِلٰى مَرْيَمَ وَرُوْحٌ مِّنْهُ ۚ فَاٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖ ۚ وَلَا تَقُوْلُوْا ثَلٰثَةٌ ۚ اِنْتَهُوْا خَيْرًا لَّكُمْ ۚ اِنَّمَا اللّٰهُ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ ۚ سُبْحٰنَهٗٓ اَنْ يَّكُوْنَ لَهٗ وَلَدٌ ۘ لَهٗ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَمَا فِى الْاَرْضِ ۚ وَكَفٰى بِاللّٰهِ وَكِيْلًا ﴿١٧١﴾ ع

171. Enyi watu wa Kitabu! Msipindukie mipaka katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo kweli. Masihi Isa bin Maryamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na (ni kiumbe aliyeumbwa kwa) tamko lake (tu Mwenyezi Mungu) alilompelekea Maryamu. Na ni roho iliyotoka Kwake (Mwenyezi Mungu kama roho nyengine). Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume yake; wala msiseme "watatu . . ." Jizuieni (na itikadi hiyo); itakuwa bora kwenu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mungu Mmoja tu. Ni mbali na utakatifu wake kuwa ana mwana. Ni vyake (vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa kutosha.

لَنْ يَّسْتَنْكِفَ الْمَسِيْحُ اَنْ يَّكُوْنَ عَبْدًا لِّلّٰهِ وَلَا الْمَلٰٓئِكَةُ الْمُقَرَّبُوْنَ ۚ وَمَنْ يَّسْتَنْكِفْ عَنْ عِبَادَتِهٖ وَيَسْتَكْبِرْ فَسَيَحْشُرُهُمْ اِلَيْهِ جَمِيْعًا ﴿١٧٢﴾

172. Masihi (Nabii Isa) hataona unyonge kuwa mja wa Mwenyezi Mungu, wala Malaika waliokurubishwa (na Mwenyezi Mungu hawataona unyonge kuwa waja wa Mwenyezi Mungu). Na watakaouona unyonge uja wa Mungu na kutakabari, basi atawakusanya wote Kwake (awatie Motoni).

---

kuwa ni Mtume wake; basi kukanusha kwa hao wanaokanusha hakuna maana.

171-172. Wanafunukiwa macho Manasara na kuonyeshwa upotofu walio nao wa kumwitakidi Nabii Isa (a) Mungu au (b) Mtoto wa Mungu au (c) Mmoja katika waungu watatu.

فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُوَفِّيهِمْ
أُجُورَهُمْ وَيَزِيدُهُمْ مِنْ فَضْلِهِ ۖ وَأَمَّا الَّذِينَ اسْتَنْكَفُوا
وَاسْتَكْبَرُوا فَيُعَذِّبُهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ۙ وَلَا يَجِدُونَ
لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿١٧٣﴾

173. Na ama wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, basi atawapa ujira wao (sawa sawa), na kuwazidishia kwa fadhila Zake. Lakini wale walioona unyonge na kufanya kiburi, basi atawaadhibu kwa adhabu iumizayo, wala hawatapata rafiki wala msaidizi (yo yote) mbele ya Mwenyezi Mungu.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ بُرْهَانٌ مِنْ رَبِّكُمْ
وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ نُورًا مُبِينًا ﴿١٧٤﴾

174. Enyi watu! Imekufikieni dalili kutoka kwa Mola wenu, na tumekuteremshieni nuru iliyo dhahiri.

فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَاعْتَصَمُوا بِهِ فَسَيُدْخِلُهُمْ فِي
رَحْمَةٍ مِنْهُ وَفَضْلٍ وَيَهْدِيهِمْ إِلَيْهِ صِرَاطًا
مُسْتَقِيمًا ﴿١٧٥﴾

175. Ama wale waliomwamini Mwenyezi Mungu na kumshika (sawa sawa), basi hao atawaingiza katika rehema Zake na fadhila (Zake) na kuwaongoza kwake kwa njia iliyonyoka.

يَسْتَفْتُونَكَ ۖ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِي الْكَلَالَةِ ۚ
إِنِ امْرُؤٌا هَلَكَ لَيْسَ لَهُ وَلَدٌ وَلَهُ أُخْتٌ
فَلَهَا نِصْفُ مَا تَرَكَ ۚ وَهُوَ يَرِثُهَا إِنْ لَمْ يَكُنْ لَهَا
وَلَدٌ ۚ فَإِنْ كَانَتَا اثْنَتَيْنِ فَلَهُمَا الثُّلُثَانِ مِمَّا تَرَكَ ۚ
وَإِنْ كَانُوا إِخْوَةً رِجَالًا وَنِسَاءً فَلِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ
الْأُنْثَيَيْنِ ۗ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ أَنْ تَضِلُّوا ۗ وَاللَّهُ
بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٧٦﴾

176. Wanakuuliza, sema: "Mwenyezi Mungu anakupeni hukumu juu ya mkiwa. Kama mtu amekufa, hali hana mtoto, lakini anaye dada; basi atapata (huyo dada) nusu ya yale aliyoyaacha (maiti). Na yeye (mtu huyu) atamrithi (dada yake) ikiwa hana mwana. Na kama wao ni (madada) wawili, basi watapata thuluthi mbili za yale aliyoyaacha. Na wakiwa ndugu wanaume na wanawake, basi (kila) mwanamume (mmoja) atapata sehemu iliyo sawa na ya wanawake wawili. Mwenyezi Mungu anakubainishieni ili msipotee; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

---

176. Mkiwa ni maiti asiyeacha mzee wala mtoto wala mjukuu ila kaacha ndugu.
Na ndugu waliokusudiwa hapa ni ndugu wa kwa (a) baba mmoja mama mmoja au wa (b) kwa baba tu. Ndugu wa kwa mama umetajwa uriihi wao katika Aya ya 12 ya Sura hii hii.



Ina Aya 120 **SURAT AL - MAIDAH** *Ina Makara 16*

(Imeteremka Madina)

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَوْفُوْا بِالْعُقُوْدِ ۭ اُحِلَّتْ لَكُمْ بَهِيْمَةُ الْاَنْعَامِ اِلَّا مَا يُتْلٰى عَلَيْكُمْ غَيْرَ مُحِلِّي الصَّيْدِ وَاَنْتُمْ حُرُمٌ ۭ اِنَّ اللّٰهَ يَحْكُمُ مَا يُرِيْدُ ①

1. Enyi mlioamini! Tekelezeni wajibu (wenu). Mmehalalishiwa wale wanyama wenye miguu mine, ila wale mnaosomewa (kuwa ni haramu). Lakini msihalalishe kuwinda mkiwa katika Hija. Hakika Mwenyezi Mungu anahukumu apendavyo.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُحِلُّوْا شَعَاۗىِٕرَ اللّٰهِ وَلَا الشَّهْرَ الْحَرَامَ وَلَا الْهَدْيَ وَلَا الْقَلَاۗىِٕدَ وَلَآ اٰۗمِّيْنَ الْبَيْتَ الْحَرَامَ يَبْتَغُوْنَ فَضْلًا مِّنْ رَّبِّهِمْ وَرِضْوَانًا ۭ وَاِذَا حَلَلْتُمْ فَاصْطَادُوْا ۭ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ اَنْ صَدُّوْكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ اَنْ تَعْتَدُوْا ۘ وَتَعَاوَنُوْا عَلَي الْبِرِّ وَالتَّقْوٰى ۠ وَلَا تَعَاوَنُوْا عَلَي الْاِثْمِ وَالْعُدْوَانِ ۠ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ۭ اِنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ②

2. Enyi mlioamini! Msivunje hishima ya alama za (dini ya) Mwenyezi Mungu wala (hishima) ya mwezi uliotukuzwa, wala hishima ya wanyama wanaopelekwa Makka kuchinjwa, wala (hishima) ya yile wanyyotiwa (hao wanyama) vya kuonyesha kuwa wanakusudia Makka, wala (hishima) ya wale wakusudiyao kwenda kwenye Nyumba takatifu (ya Makka). (Wanakwenda huko) kutafuta fadhila za Mola wao na radhi (Yake). Na mkishatoka katika Hija yenu basi windeni (mkitaka). Wala kule kuwachukia watu kwa kuwa walikuzuilieni kufika Msikiti uliotukuzwa (wa Makka) kusikupelekeeni kuwafanyia jeuri (ili kuwalipa jeuri yao; msifanye). Na saidianeni katika wema na taqwa, wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

N.B. Imeitwa kwa jina hili la *Suratul Maida* (Sura ya Karamu) kwa ajili ya khabari ya karamu waliotaka watu wa Nabii Isa wateremshiwe mbinguni ambayo imetajwa katika Aya ya 112.

2. Katika sifa za Uislamu ni kuhishimu vinavyofanywa kwa ajili ya dini, kama hao wanyama wanaopelekwa Makka kwenda kuchinjwa na kutolewa sadaka huko.

Na wenyewe Mahujaji huwavisha vigwe wanyama hao au huwatia mapambo mengine ya kuonyesha kuwa ni wanyama wanaopelekwa Makka. Basi haipendezi kuvunja taadhima ya vigwe hivyo wala taadhima ya wanyama hao; seuze hao binaadamu wenyewe mahujaji; ndio kabisa.

Basi mahujaji hao hata wakiwa wa kikafiri ambao wakipigana na Waislamu; lakini maadamu wamo katika hija wanakwenda kwa salama basi Waislamu wasivunje taadhima ya hija yao, japokuwa makafiri hao waliwafanya mabaya hao Waislamu kabla ya hapo. Waislamu walipokuwa hawana nguvu hao makafiri walikuwa wakiwazuilia kuja Makka kuhiji. Waislamu waliwarai kila namna wawape ruhusa waingie hiyo Makka mara moja wahiji kisha wende zao. Nao walikataa na waliwazatitia vita vya kuwapiga, na wakawahi kuwadhuru baadhi yao. Na juu ya hivi Waislamu walipopata nguvu waliambiwa wasiwalipe ubaya wao. Watu hawasaidiani katika kufanya mabaya; watu husaidiana katika wema.

N.B. Makafiri walikuwa wakenda huko Makka huhiji mbele ya masanamu yao hayo waliyoyatia ndani na nje ya Al Kaaba. Mpaka katika mwaka wa 9 wa Al Hijra (bado mwaka mmoja Mtume atakufa) ndipo walipozuiliwa kuja kuhiji hija ya ukafiri.

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنْزِيرِ
وَمَآ أُهِلَّ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِۦ وَالْمُنْخَنِقَةُ
وَالْمَوْقُوذَةُ وَالْمُتَرَدِّيَةُ وَالنَّطِيحَةُ وَمَآ أَكَلَ
السَّبُعُ إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ ۖ وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ وَ
أَن تَسْتَقْسِمُوا بِالْأَزْلَٰمِ ۚ ذَٰلِكُمْ فِسْقٌ ۗ الْيَوْمَ يَئِسَ
الَّذِينَ كَفَرُوا مِن دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِ ۚ
الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ
نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَٰمَ دِينًا ۚ فَمَنِ اضْطُرَّ
فِي مَخْمَصَةٍ غَيْرَ مُتَجَانِفٍ لِّإِثْمٍ ۙ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ
رَّحِيمٌ ﴿٣﴾

3. Mmeharimishiwa nyamafu na damu na nyama ya nguruwe, na kinyama kilichochinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kilichokufa kwa kusongeka koo, na kilichokufa kwa kupigwa, na kilichokufa kwa kuanguka, na kilichokufa kwa kupigwa pembe (na mwengine), na alichokila mnyama (kikafa), ila mkiwahi kukichinja (kabla hakijafa). Na (pia mmeharimishiwa) kilichochinjwa panapofanyiwa ibada isiyokuwa ya Mungu (kama mizimuni). Na ni (haramu kwenu) kutaka kujua siri kwa kuagua kwa mabao (na yaliyo kama hayo). Hayo yote ni maasiya. Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu, basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi. Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu. Na mwenye kushurutishwa na njaa, pasipo kuelekea kwenye dhambi, (akala hivi vilivyoharimishwa, basi hapana kitu); hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha (na) Mwingi wa rehema.

---

3. Hapa vinatajwa vilivyoharimishwa kuvila: (a) Mnyama aliyekufa mwenyewe (b) Damu (c) Nyama ya nguruwe (d) Kilichochinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Kama:–

(1) Mnyama anayechinjwa kwa ajili ya kutia msingi nyumba au kisima au . . . kwa kuchelea Shetani anayekuwapo kaika kuchimba msingi.

(2) Mnyama anayechinjwa kwa ajili ya Shetani wa nyumba au wa shamba au wa mtu fulani au . . . ili asije huyo Shetani akawadhuru hao wenyewe ikiwa hatafanyiwa hayo.

(3) Mnyama anayechinjwa kuwa zindiko la mji la kila mwezi au la kila mwaka au la mwaka huu . . . kwa kuwa mwaka huu imeonekana sharti achinjwe mnyama au itafika balaa.

(4) Mnyama anayechinjwa kwa ajili ya kukiusha arusi au aliyetoka safari au . . . ili Shetani ashughlike na mnyama huyo asije na haja ya kumdhuru huyo arusi.

(5) Mnyama anayechinjwa kwa ajili ya kukiusha jeneza la mtu mkubwa au la . . . ili Shetani asichukue upesi mtu namna huyo au kuridhishwa kwa damu ya huyo mnyama.

(6) Wanyama wanaochinjwa kwa ajili ya mashindano (a) Chama. Hiki kikachinja hivi na chama hiki kikachinja hivi kwa ajili ya kupikuana tu basi au (b) Maulidi. Watu wa upande huu wakachinja hivi na wa huko wakachinja zaidi ili wawashinde hao tu basi Au (c) Bwana fulani kachinja hivi katika arusi yake au jando lake au matanga ya mtu au . . . na bwana fulani akachinja zaidi si kwa sababu yo yote ila kuzidiana na kufakharishana.

Basi wanyama wote hawa huwa ni Najisi, Haramu kuwala.

Na tangu pale iliposemwa 'Kilichokufa kwa kupigwa na kilichokufa . . . ila mkiwahi kukichinja' ni kuonyesha kuwa kinyama cha kuliwa kikifikilia hali ya umaiti kwa sababu yo yote ile, kama vile kupondwa na gari au nyinginezo—lakini bado hakijatoka roho—kikidirikiwa, basi kitafaa kuliwa.

Na iliposemwa 'Kama mizimuni' basi vile vile makaburini. Kuweka nadhiri ya kuchinja mnyama kaburini kwa fulani atakapopata jambo fulani, nadhiri hiyo haisihi na nyama hiyo ni Najisi, Haramu kuliwa.

Na kutazamia kumetajwa pia hapa kuwa ni haramu kutazamia kokote kutakokuwako—kukiwa kwa ubao, kwa mchanga, kwa kaure, kwa tasbihi, kwa vitabu na mengineyo. Mambo ya kutazamia yamekatazwa tu.

Leo hii iliyokaririwa kutajwa hapa ni leo ya Ijumaa mwezi 9 Mfanguo tatu mwaka 10 wa Al Hijra (na mwaka wa 23 tangu kupewa Utume). Siku hiyo ndiyo kazi ya Mtume imekuwa imekwishakamilika—kishafikisha kila alilotaka Mwenyezi Mungu afikishe. Na siku hiyo ndipo makafiri tamaa yao ilipowatamauka—tamaa ya kuona kuwa dini hii haitasimama, itakufa njiani kwa kuwa wao wakubwa wamepinga; haikufuatwa ila na chipukizi na watu madhaifu. Lakini siku ile walipoona nguvu zile za Uislamu walitambua kwa yakini kuwa hila zao hazikufaa kitu.

يَسْـَٔلُونَكَ مَاذَآ أُحِلَّ لَهُمْ ۖ قُلْ أُحِلَّ لَكُمُ
الطَّيِّبَٰتُ ۙ وَمَا عَلَّمْتُم مِّنَ الْجَوَارِحِ مُكَلِّبِينَ تُعَلِّمُونَهُنَّ
مِمَّا عَلَّمَكُمُ اللَّهُ ۖ فَكُلُوا مِمَّآ أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَاذْكُرُوا
اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٤﴾

4. Wanakuuliza wamehalalishiwa nini. Sema: "Mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri na mlichowafunza wanyama (kukiwinda) na ndege wa mawindo (kukiwinda). Mnawafunza alivyokufunzeni Mwenyezi Mungu. Basi kuleni walichokukamatieni, na mkisomee jina la Mwenyezi Mungu. Na mwogopeni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.

اَلْيَوْمَ أُحِلَّ لَكُمُ الطَّيِّبَٰتُ ۖ وَطَعَامُ الَّذِينَ أُوتُوا
الْكِتَٰبَ حِلٌّ لَّكُمْ ۖ وَطَعَامُكُمْ حِلٌّ لَّهُمْ ۖ وَالْمُحْصَنَٰتُ
مِنَ الْمُؤْمِنَٰتِ وَالْمُحْصَنَٰتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا
الْكِتَٰبَ مِن قَبْلِكُمْ إِذَآ ءَاتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ مُحْصِنِينَ

5. Leo mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri. Na chakula cha wale waliopewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali kwao. Na (mmehalalishiwa kuwaoa) wanawake wema wa Kiislamu na wanawake wema katika wale waliopewa Kitabu kabla yenu. (Ni halali kwenu kuwaoa),

---

Mambo yote ni ya Mungu
Ndiye pweke Mwenye quwa

Atakalo ndilo huwa
Mwenye amri na Shani

Na imetajwa hapa kuwa yale ya haramu ya kula (a) Mizoga (b) Damu (c) Nyama ya nguruwe (d) Vilivyochinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu . . . hupatikana ruhusa kuliwa, mtu anapobanwa na njaa ya kumtoa roho. Hapo itamjuzia kula kiasi cha kuondosha ile njaa ya kumtoa roho.

Katika hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 4 ya *Suratul Maida* wamejidai kutilia hivi: "Injili yenyewe inaahidi kufika kwa Mtume mwingine ambaye atawongoza watu kwenye haki yote." Wamekitia kipande hiki, na-hali ya kuwa hawamkusudii Mtume Muhammad, kama alivyobainisha Mwenyewe Mwenyezi Mungu katika Aya zake za Qurani kama Aya ya 156 ya *Suratul Aaraf* na Aya ya 6 ya *Suratus Saf.* Wao wanataka awe huyo mtu wao. Hatutawacha muradi wa Mwenyezi Mungu, tukaufuata muradi wao mwovu.

4. Ndege na Nyama waliohalalishwa kuwawinda, wakawindwa na madege wenziwao au wanyama wengineo (waliofundishwa kuwinda), wakafa ndege hao au wanyama hao kwa vishindo na mibano ya hao ndege au wanyama waliowawinda, itafaa kuliwa japo hawajawahi kuchinjwa, maadamu wamewakuta wamekwishakufa.

Ama wakiwakuta wahai bado watawachinja.

N.B.—Na ndege na wanyama waliohalalishwa kuwindiwa ni wale wenye meno makali au makucha makubwa makali.

Na vile vile akiwindwa mnyama au ndege kwa mishare au mikuki akafa itafaa kuliwa japo hakuchinjwa; ila akimkuta yu hai ndiyo sharti amchinje.

N.B. Na kila kuwinda kwa kitu chenye makali hukumu yake ni hii:- Kikifa kwa makali yale kitaliwa japo hakuwahi kumchinja.

Ama kinachowinda kikaua kwa uzito wake, kama jiwe—au kikaua moto wake—kama bunduki—basi kinyama hicho au ndege huyo haliwi akifa kwa kuwindwa huko; ila akutikane yu hai achinjwe; hapo ndiyo itasihi kuliwa. Lakini akifa kwa ule moto tu wa bunduki au kwa ule uzito tu wa jiwe basi hataliwa—anakuwa najisi, haramu kuliwa; ila kwa madhehebu ya Kimaliki; wao wanasema inafaa kuliwa mnyama anayekufa kwa kupigwa kwa bunduki.

Kama ilivyohalalishwa kula vinavyochinjwa kwa visu na kwa vyenye MAKALI zaidi kuliko visu, vikafa kwa makali haya; basi ndivyo inavyokubalishwa kula vilivyo kufa kwa makucha au kwa meno ya wanyama au ndege wenye makucha namna hiyo na meno namna hayo, na wakafundishwa kuwindia kwa hayo, kama simbamarara na tai na walio kama hawa. Mnyama wanayemtia mbaroni hao, wakamwua kwa kucha zao au meno yao, akafika huyo mwenyewe akamkuta mikononi mwao kisha kufa, ataliwa bila ya kuchinjwa. Ama akimkuta yu hai, hapo itapasa amchinje.

Na sharti ya kuchinja kwa madhehebu ya Kishafi ni moja tu—kumkata kwa upesi njia ya kupitia chakula na njia ya kupitia pumzi. Mengine yote yaliyosalia ni Suna, kama (a) kumwelekeza kibla, (b) kupiga *Bismillahi,* (c) kisu kuwa kikali sana, (d) kumlaza mahala pasipoumiza, na (e) kwa namna isiyoumiza na yaliyo kama haya.

Ama kusema kuwa:- (a) Mwanamke hawezi kuchinja sharti atahiriwe (b) Na kisu sharti kiwe kina mpini . . . Haya ni maneno ya upuzi. Mwislamu yo yote anayejua kuchinja akachinja kinachojuzu kuliwa, kitaliwa.

N.B. Na ulama wengi hata wasiokuwa wa Kimaliki wameridhia kauli hiyo sasa.

غَيْرَ مُسٰفِحِيْنَ وَلَا مُتَّخِذِيْٓ اَخْدَانٍ ۭ وَمَنْ يَّكْفُرْ
بِالْاِيْمَانِ فَقَدْ حَبِطَ عَمَلُهٗ ۠ وَهُوَ فِي الْاٰخِرَةِ مِنَ
الْخٰسِرِيْنَ ۝ ع ۵

mtakapowapa mahari yao, mkafunga nao ndoa, bila kufanya uzinzi (kwa mwanamke huyu na huyu), wala kuwaweka (wanawake wa) kinyumba. Na anayekataa kuamini bila shaka amali zake (za kheri) zimepotea na yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa wenye khasara.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِذَا قُمْتُمْ اِلَى الصَّلٰوةِ فَاغْسِلُوْا
وُجُوْهَكُمْ وَاَيْدِيَكُمْ اِلَى الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوْا بِرُءُوْسِكُمْ وَ
اَرْجُلَكُمْ اِلَى الْكَعْبَيْنِ ۭ وَاِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوْا ۭ
وَاِنْ كُنْتُمْ مَّرْضٰٓى اَوْ عَلٰي سَفَرٍ اَوْ جَاۗءَ اَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ
الْغَاۗىِٕطِ اَوْ لٰمَسْتُمُ النِّسَاۗءَ فَلَمْ تَجِدُوْا مَاۗءً فَتَيَمَّمُوْا
صَعِيْدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوْا بِوُجُوْهِكُمْ وَاَيْدِيْكُمْ مِّنْهُ ۭ مَا
يُرِيْدُ اللّٰهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِّنْ حَرَجٍ وَّلٰكِنْ يُّرِيْدُ
لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهٗ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ۝
وَاذْكُرُوْا نِعْمَةَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَمِيْثَاقَهُ الَّذِيْ

6. Enyi mlioamini! Mnaposimama ili mkasali, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na (osheni) miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba basi ogeni. Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake, na hamkupata maji, basi kusudieni (tayamamuni) udongo (mchanga) ulio safi na kuupaka nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu; bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema Yake juu yenu ili mpate kushukuru.

7. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, na ahadi Yake aliyofungamana nanyi,

---

5. Chakula cha kuchinja hakiwi halali kwa Waislamu ila kichinjwe na (a) Mwislamu au kichinjwe na (b) Myahudi au (c) Mnasara, kwa sharti ile ya kuchinja—sio kuwanyonga.

Ama wasiokuwa hawa hakiwi halali wanachokichinja.

Ama chakula kisichokuwa cha kuchinja ni halali kwa Mwislamu kukila hata kikitengenezwa na makafiri, kwa madhehebu ya Kisuni maadamu (a) Hujaona kuwa kimeingia najisi wala (b) Si katika vile vyakula vilivyokatazwa katika Uislamu.

Na ni halali kwa mwanamume Mwislamu kumwoa

(a) Mwanamke wa Kiislamu au

(b) Mwanamke wa Kiyahudi au

(c) Mwanamke wa Kinasara—maadamu ukoo wao umeingia katika dini hizo kabla ya Uislamu haujakuja.

N.B.—Ama hawa wanaoitwa Misheni wanaoingia katika Ukristo sasa si halali kuwaoa. Ni haramu wala ndoa haisihi.

N.B.—Ama mwanamke wa Kiislamu hana ruhusa kuolewa ila na Mwislamu tu basi.

Na hapa imekatazwa habari ya kuzini. Basi ikiwa kuzini kwa Kinyumba au Kuchupia huku na Kuchupia huko. Zote hizo ni zina; zimeharimishwa.

Sharti mtu amwoe mwanamke kwa sharti zake. Nazo ni hizi:—

(a) Kukubali huyo mwenyewe mwanamke

(b) Wali wake huyo mwanamke atoe idhini ampe mtu amwoze huyo mume au mwenyewe huyo wali amwambie huyo mume 'Nimekuoza Fulani binti Fulani'

(c) Kuitikia mume kuwa 'Nimekubali kumwoa Fulani binti Fulani'

(d) Mashahidi kushuhudia haya. Uchache wake wanaume wawili wenye hishima zao mbele ya watu.

6. Hapa zimetajwa nguzo za kutawadha—viungo vya kuviosha. Navyo ni 4. Na imetajwa ya kuwa yanapokosekana maji—au anapozuiliwa kuyatumia maji kwa ajili ya ugonjwa—basi atumie mchanga (atayamamu); avipake mchanga huo viungo viwili tu (a) Uso na (b) Mikono miwili.

N.B.—Habari ya Kutayamamu imetajwa kwa urefu katika maelezo ya Aya ya 43 ya *Suratin Nisaa.*

Na imetajwa kwamba mtu akiwa na janaba naakoge. Na sharti ya kukoga ni

(a) Kutia nia moyoni mwako kuwa unaoga kuondoa janaba na

(b) Kukieneza maji kiwiliwili chote.

Na janaba inapatikana kwa moja katika mawili.

(a) Kuingiliana Kila mmoja ataoga—aliyeingilia na aliyeingiliwa, akiwa mwanamke au akiwa mwanamume pia.

mliposema: "Tumesikia na tunatii." Na mwogopeni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu hujua (hata) yaliyomo vifuani.

وَاثَقَكُمْ بِهٖٓ ۙ اِذْ قُلْتُمْ سَمِعْنَا وَاَطَعْنَا ۫ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ۭ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ۝

8. Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi (wa kupitisha haki) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, muwe mkitoa shahada kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia insafu (uadilifu). Fanyeni uadilifu; huko ndiko kunakomkurubisha mtu na ucha-Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) mnayoyatenda.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُوْنُوْا قَوّٰمِيْنَ لِلّٰهِ شُهَدَاۗءَ بِالْقِسْطِ ۡ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ عَلٰٓي اَلَّا تَعْدِلُوْا ۭ اِعْدِلُوْا ۣ هُوَ اَقْرَبُ لِلتَّقْوٰى ۡ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ۭ اِنَّ اللّٰهَ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ۝

9. Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini na kufanya vitendo vizuri (ya kwamba) watapata msamaha na malipo makubwa.

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ۙ لَهُمْ مَّغْفِرَةٌ وَّاَجْرٌ عَظِيْمٌ ۝

10. Na waie waliokufuru na kuzikadhibisha Aya zetu, hao ndio watu wa Motoni.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَآ اُولٰۗىِٕكَ اَصْحٰبُ الْجَحِيْمِ ۝

11. Enyi mlioamini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu. (Kumbukeni) waliponuia watu kukunyosheeni mikono yao, akaizuilia mikono yao kufika kwenu. Na mwogopeni Mwenyezi Mungu. Na (maadamu watu wanaamini) basi wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اذْكُرُوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ اِذْ هَمَّ قَوْمٌ اَنْ يَّبْسُطُوْٓا اِلَيْكُمْ اَيْدِيَهُمْ فَكَفَّ اَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ۭ وَعَلَي اللّٰهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُوْنَ ۝ ع

12. Na Mwenyezi Mungu alifunga ahadi na wana wa Israili (Mayahudi). Na tukawawekea miongoni mwao wakubwa kumi na mbili. Na Mwenyezi Mungu akasema: "Kwa yakini mimi ni pamoja nanyi. Kama mkisali na kutoa Zaka na mkiwaamini Mitume wangu na kuwasaidia na kumpa Mwenyezi Mungu karadha iliyo nzuri (kwa kutoa katika njia za kheri na kusaidia masikini), bila shaka nitakufutieni maovu yenu na kukuingizeni katika Mabustani ipitayo mito mbele yake. Lakini atakayekataa miongoni mwenu baada ya (ahadi) hii, bila shaka amepotea njia iliyo sawa."

وَلَقَدْ اَخَذَ اللّٰهُ مِيْثَاقَ بَنِيْٓ اِسْرَاۗءِيْلَ ۚ وَبَعَثْنَا مِنْهُمُ اثْنَيْ عَشَرَ نَقِيْبًا ۭ وَقَالَ اللّٰهُ اِنِّىْ مَعَكُمْ ۭ لَىِٕنْ اَقَمْتُمُ الصَّلٰوةَ وَاٰتَيْتُمُ الزَّكٰوةَ وَاٰمَنْتُمْ بِرُسُلِيْ وَعَزَّرْتُمُوْهُمْ وَاَقْرَضْتُمُ اللّٰهَ قَرْضًا حَسَنًا لَّاُكَفِّرَنَّ عَنْكُمْ سَيِّاٰتِكُمْ وَلَاُدْخِلَنَّكُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ۚ فَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاۗءَ السَّبِيْلِ ۝

13. Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, tuliwalani na tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu (hazisikii kheri. Wamekuwa) Wanayabadilisha maneno (ya Mwenyezi Mungu yaliyo katika Taurati na Injili) na mahali pake. Na wameacha sehemu (kubwa) ya yale

فَبِمَا نَقْضِهِمْ مِّيْثَاقَهُمْ لَعَنّٰهُمْ وَجَعَلْنَا قُلُوْبَهُمْ قٰسِيَةً ۚ يُحَرِّفُوْنَ الْكَلِمَ عَنْ مَّوَاضِعِهٖ ۙ وَنَسُوْا حَظًّا مِّمَّا ذُكِّرُوْا بِهٖ ۚ وَلَا تَزَالُ

(b) Kutoka manii japokuwa si kwa kuingiliana; kama kulala ukaona manii kitandani mwako.

N.B.—Ama kuota unafanya kitendo, na ulipoamka usione manii juu ya kitanda, basi haipasi kuoga.

8. Maamrisho haya ni kama yale yaliyo katika Aya ya 135 ya *Suratun Nisaa*, rejea yaliyosemwa huko.

11. Mwenyezi Mungu anawakumbusha Waislamu baadhi ya balaa alizowafungua nazo ili Washukuru na wamtegemee yeye, si mizimu na makaburi.

تَطَّلِعُ عَلٰى خَآئِنَةٍ مِّنْهُمْ اِلَّا قَلِيْلًا مِّنْهُمْ
فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاصْفَحْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٣﴾

waliyokumbushwa. Na utaendelea kupata khabari za khiana yao, isipokuwa wachache miongoni mwao. Basi wasamehe na waache. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema (japokuwa wanafanyiwa mabaya).

وَمِنَ الَّذِيْنَ قَالُوْٓا اِنَّا نَصٰرٰٓى اَخَذْنَا مِيْثَاقَهُمْ
فَنَسُوْا حَظًّا مِّمَّا ذُكِّرُوْا بِهٖ ۠ فَاَغْرَيْنَا بَيْنَهُمُ الْعَدَاوَةَ
وَالْبَغْضَآءَ اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ ؕ وَسَوْفَ يُنَبِّئُهُمُ اللّٰهُ بِمَا
كَانُوْا يَصْنَعُوْنَ ﴿١٤﴾

14. Na kwa wale waliosema: "Sisi ni Wakristo," tulichukua ahadi kwao, lakini wakaacha sehemu (kubwa) ya yale waliyokumbushwa, kwa hivyo tukaweka baina yao (wenyewe kwa wenyewe) uadui na bughudha mpaka siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu atawaambia waliyokuwa wakiyafanya.

يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ قَدْ جَآءَكُمْ رَسُوْلُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ
كَثِيْرًا مِّمَّا كُنْتُمْ تُخْفُوْنَ مِنَ الْكِتٰبِ وَيَعْفُوْا عَنْ
كَثِيْرٍ ؕ قَدْ جَآءَكُمْ مِّنَ اللّٰهِ نُوْرٌ وَّكِتٰبٌ مُّبِيْنٌ ﴿١٥﴾

15. Enyi watu wa Kitabu! Amekwisha kufikieni Mtume wetu, anayekudhihirishieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na husamehe mengi. Bila shaka imekwisha kufikieni nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Kitabu kinachobainisha (kila jambo).

يَّهْدِيْ بِهِ اللّٰهُ مَنِ اتَّبَعَ رِضْوَانَهٗ سُبُلَ
السَّلٰمِ وَيُخْرِجُهُمْ مِّنَ الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوْرِ
بِاِذْنِهٖ وَيَهْدِيْهِمْ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿١٦﴾

16. Kwa (kitabu) hicho Mwenyezi Mungu huwaongoza wenye kufuata radhi Yake katika njia za salama, na huwatoa katika kiza kuwapeleka katika nuru kwa amri Yake, na huwaongoza katika njia iliyonyoka.

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِيْنَ قَالُوْٓا اِنَّ اللّٰهَ هُوَ الْمَسِيْحُ
ابْنُ مَرْيَمَ ؕ قُلْ فَمَنْ يَّمْلِكُ مِنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا اِنْ
اَرَادَ اَنْ يُّهْلِكَ الْمَسِيْحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَاُمَّهٗ وَمَنْ

17. Kwa yakini wamekwisha kufuru wale waliosema: "Mwenyezi Mungu ni Masihi bin Maryamu." Sema: "Ni nani atakayemiliki (kuzuilia) cho chote mbele ya Mwenyezi Mungu kama yeye

---

13. Yanatajwa baadhi ya mabaya ya Mayahudi. Moja katika hayo ni kubadilisha maneno ya kitabu chao alichowateremshia Mwenyezi Mungu, wakatoa wasiyoyataka, wakatia wanayoyapenda. Na kazi hii pia Manasara waliifanya na wanaifanya mpaka leo. Hizi Biblia zao wanazozitabiisha wakazitawanya katika pande zetu hizi na kwingineko. Ukiitazama Chapa ya safari hii utaiona tafauti kidogo na ya safari ile. Na kila inayokuja inakhitalifiana na iliyotangulia; ima (a) yametolewa yaliyokuwamo au (b) yametiwa yasiyokuwamo au (c) yanasemwa vingine si kama ilivyosemwa mara ya awali. Na yote haya yanaonyesha dhahiri shahiri kuwa hiyo ni mipango yao wenyewe tu ya kutaka kuvutia kwa pupa upande wa dini yao. Wanayoyaona yatawavuta watu wanayatia—wakasema ni ya Mungu; kumbe yao wenyewe—na wanayoyaona yatawakirihbiza watu wanayatoa upesi upesi, wakayazikilia mbali. Dini gani hiyo inayogeuka kila usiku uchao na mchana uingiyao!

14. Kuonyesha huo ugomvi mkubwa kabisa na kukufurishana kuliko baina ya madhehebu ya Kinasara kama—Roman Catholics, Protestants, Orthodox na wengineo—ni kwa ajili ya kule kutupa kwao mafundisho ya haki aliyowapa Mtume mtukufu Nabii Isa na kitabu alichokuja nacho.

Akisema mtu: "Na Waislamu wana madhehebu mbali mbali;" atajibiwa lakini hayakufurishani madhehebu hayo, yanaingiliana katika misikiti yao na kusali pamoja tukichukua mfano Unguja tutaona: (a) Msikiti Ijumaa mkongwe wa Forodhani unaosaliwa na Suni kaujenga Ibadhi mwenye kabila ya Muharmy akawapa Suni. Na akawajengea wenye madhehebu ya Kiibadhi kama huo katika mtaa wa Baghani. (b) Msikiti Ijumaa mkubwa wa Malindi kaujenga Kadhi wa Kisunni — Sheikh Muhyiddin — kwa msaada mkubwa kabisa wa Seyyid Majid (Ibadhi). (c) Msikiti wa Hamamuni wanaosalia Ibadhi kaujenga Sunni, katika Mashatry. (d) Msikiti wanaosali Shia Ithnaashariyya Kiponda, kawapa kiwanja Sayyid Hamed bin Thuweyny (Ibadhi). (e) Msikiti mkubwa wa Miembeni unaosaliwa na Suni kaujenga Shia Dawudiyya (bohora). (f) Baadhi ya Misikiti mikubwa ya Makunduchi inayosaliwa na Suni kaijenga Shia Ithnaashariyya. (g) Msikiti wa Hollis Road unaosaliwa na Sunni kaujenga Shia Ismailiyya. (h) Msikiti wa Gulioni unasaliwa na Sunni umejengwa na Khoja Ismailiyya.

Basi khitilafu za madhehebu ya Kiislamu si za kukufurishana, na ni khitilafu ndogo tu ambazo lazima watu

فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ۚ وَ لِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ
وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۚ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ ۚ
وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ⑰

angetaka kumwangamiza Masihi mtoto wa Maryamu, na mama yake na vyote vilivyomo katika ardhi? Na ufalume wa mbinguni na ardhi na vilivyomo kati yake ni wa Mwenyezi Mungu (tu peke yake). Huumba apendavyo. Na Mwenyezi Mungu ni Mweza juu ya kila kitu.

وَ قَالَتِ الْيَهُوْدُ وَالنَّصٰرٰى نَحْنُ اَبْنٰٓؤُا اللّٰهِ
وَاَحِبَّآؤُهٗ ۚ قُلْ فَلِمَ يُعَذِّبُكُمْ بِذُنُوْبِكُمْ ۚ بَلْ
اَنْتُمْ بَشَرٌ مِّمَّنْ خَلَقَ ۚ يَغْفِرُ لِمَنْ يَّشَآءُ
وَيُعَذِّبُ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَ لِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ
وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۡ وَاِلَيْهِ الْمَصِيْرُ ⑱

18. Na Mayahudi na Wakristo wanasema: "Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na wapenzi wake." Sema: "Basi kwa nini anakuadhibuni kwa ajili ya dhambi zenu? Bali nyinyi ni watu (tu) katika aliowaumba. Humghufiria amtakaye (anapotubia) na humuadhibu amtakaye (asipotubia). Na ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake ni wa Mwenyezi Mungu. Na marejeo ni Kwake (tu)."

يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ قَدْ جَآءَكُمْ رَسُوْلُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ
عَلٰى فَتْرَةٍ مِّنَ الرُّسُلِ اَنْ تَقُوْلُوْا مَا جَآءَنَا مِنْ
بَشِيْرٍ وَّلَا نَذِيْرٍ ۡ فَقَدْ جَآءَكُمْ بَشِيْرٌ وَّنَذِيْرٌ ۗ
وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ⑲ ع

19. Enyi watu wa Kitabu! Bila shaka amekufikieni Mtume wetu, anayekubainishieni; (amekufikieni) katika wakati usio na Mitume, msije kusema: "Hakufika kwetu mtoaji wa habari njema wala mwonyaji." Basi amekufikieni abashirie na aonyaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mweza juu ya kila kitu.

وَ اِذْ قَالَ مُوْسٰى لِقَوْمِهٖ يٰقَوْمِ اذْكُرُوْا نِعْمَةَ
اللّٰهِ عَلَيْكُمْ اِذْ جَعَلَ فِيْكُمْ اَنْۢبِيَآءَ وَجَعَلَكُمْ
مُّلُوْكًا ۖ وَّاٰتٰىكُمْ مَّا لَمْ يُؤْتِ اَحَدًا مِّنَ
الْعٰلَمِيْنَ ⑳

20. Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake. "Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, alipowafanya Manabii kwenu (wenyewe) na akakufanyeni watawala (kujimiliki nafsi zenu baada ya kuwa wadhalilifu chini ya ufalme wa Firauni), na akakupeni ambayo hakuwapa wo wote katika walimwengu (wa zama zenu)."

---

wakhitalifiane. Makadiani ndio si waislamu, wamejipa wenyewe mtume wao aliyepewe utume baada ya Nabii Muhammed na mtu anayeamini hivi ni kafiri, si Mwislamu.

15. Wanaambiwa Mayahudi na Manasara waache kuficha sasa, kwani waliyokuwa wakiyaficha yamekwisha kufichuka kwa kuja Qurani; waifuate nuru hiyo waongoze njia ya haki.

17. Wanatajiwa ukafiri wao wa kumfanya Nabii Isa (a) Mtoto wa Mungu au (b) Mungu mwenyewe au (c) Mmoja katika hao waungu watatu. Na wanatajiwa udhaifu wa Nabii Isa mbele ya Mwenyezi Mungu kama udhaifu wa viumbe vyengine. Na kubainishwa kuwa Mwenyezi Mungu anaumba anavyotaka Mwenyewe. Si ajabu kumwumba Nabii Isa bila ya baba wala si ajabu kumwumba Nabii Adamu bila ya baba wala mama.

Na vipi Wakristo wakamuona Nabii Isa ni mtoto wa Mungu kwa kuwa hana baba; na kwa nini wasimuitakidi Nabii Adamu naye kuwa mtoto wa Mungu, na hali ya kuwa yeye hana baba wala mama pia? Watu wakikosa inapasa wakiri warejee kuifuata haki; wasiwe na kinyongo katika kuifuata haki.

19. Wanaondoshewa udhuru kuwa hawana tena udhuru. Mambo meupe haya.

20. Wanakumbushwa Mayahudi neema kubwa kabisa alizowapa Mwenyezi Mungu. Mtume alikuwa akisema: "Mtu akipambazukiwa, yumo katika amani yeye na watu wake wote, na wote wana afya nzuri, na wanacho cha kukila na cha kuvaa na pa kukaa, ndiyo amekwisha kumiliki dunia yote." Basi na wao wote takriba walifikilia katika daraja hiyo. Na wengi kabisa katika sisi ni vivi hivi. Basi natushukuru kweli kweli na aseme kila mmoja katika sisi:

Wallahi Bilahi Sikuyawaza

يٰقَوْمِ ادْخُلُوا الْاَرْضَ الْمُقَدَّسَةَ الَّتِيْ كَتَبَ
اللّٰهُ لَكُمْ وَلَا تَرْتَدُّوْا عَلٰٓى اَدْبَارِكُمْ فَتَنْقَلِبُوْا
خٰسِرِيْنَ ﴿٢١﴾

21. "Enyi watu wangu! Ingieni katika hiyo ardhi iliyotakaswa ambayo Mwenyezi Mungu amekuandikieni (Nayo ni nchi ya Shamu ambayo ilikuwa imemilikiwa na makafiri mashujaa—makanani). Wala msirudi nyuma, msije mkawa wenye kukhasirika."

قَالُوْا يٰمُوْسٰٓى اِنَّ فِيْهَا قَوْمًا جَبَّارِيْنَ ۖ وَاِنَّا لَنْ
نَّدْخُلَهَا حَتّٰى يَخْرُجُوْا مِنْهَا ۚ فَاِنْ يَّخْرُجُوْا مِنْهَا
فَاِنَّا دٰخِلُوْنَ ﴿٢٢﴾

22. Wakasema: "Ewe Musa! Huko kuna watu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka watoke humo; wakitoka humo hapo tutaingia."

قَالَ رَجُلٰنِ مِنَ الَّذِيْنَ يَخَافُوْنَ اَنْعَمَ اللّٰهُ عَلَيْهِمَا
ادْخُلُوْا عَلَيْهِمُ الْبَابَ ۚ فَاِذَا دَخَلْتُمُوْهُ فَاِنَّكُمْ
غٰلِبُوْنَ ۚ وَعَلَى اللّٰهِ فَتَوَكَّلُوْٓا اِنْ كُنْتُمْ
مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٢٣﴾

23. Watu wawili miongoni mwa wale waliomwogopa (Mungu) ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha, walisema (kuwaambia wenzao): "Waingilieni katika hilo lango (la nchi yao); maana mtakapowaingilia hapo, kwa yakini nyinyi mtashinda. Na tegemeeni juu ya Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni wenye kuamini."

قَالُوْا يٰمُوْسٰٓى اِنَّا لَنْ نَّدْخُلَهَآ اَبَدًا مَّا دَامُوْا
فِيْهَا فَاذْهَبْ اَنْتَ وَرَبُّكَ فَقَاتِلَآ اِنَّا
هٰهُنَا قٰعِدُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Wakasema: "Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane, sisi tutakaa hapa (kungojea nini litakalokuwa)."

قَالَ رَبِّ اِنِّيْ لَآ اَمْلِكُ اِلَّا نَفْسِيْ وَاَخِيْ فَافْرُقْ
بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْقَوْمِ الْفٰسِقِيْنَ ﴿٢٥﴾

25. (Musa) akasema: "Mola wangu! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu; basi tutenge na hawa mafasiki (usituhisabu kuwa tuko pamoja nao)."

قَالَ فَاِنَّهَا مُحَرَّمَةٌ عَلَيْهِمْ اَرْبَعِيْنَ سَنَةً ۚ
يَتِيْهُوْنَ فِي الْاَرْضِ ۗ فَلَا تَاْسَ عَلَى الْقَوْمِ ع
الْفٰسِقِيْنَ ﴿٢٦﴾

26. (Mwenyezi Mungu) akasema: "Basi wameharimishiwa (ardhi) hiyo kwa (muda wa) miaka arubaini; watatangatanga (mumu humu) ardhini (jangwani muda wote huo). Basi usihuzunike juu ya watu maasi."

Na moyoni mwangu
Haya ni ya Mola
Aliyonijazi

Sikulekeza
Yake majaza
Mola Rahima

Wamejidai Makadiyani kutia katika Aya waliyoita ya 21 maneno haya: "Hapa neema mbili za Mwenyezi Mungu zimetajwa: (a) Neema ya kiroho—Unabii; (b) Neema ya kidunia—Ufalme." Wameita haya ili wamthibitishie Utume mtu wao wakasema kuwa Utume unaendelea maisha kama ufalme.

Na wanaona hapo katika hiyo Aya kuwa habari hii ni kumbukumbu (kumbusho) za zamani, wanakumbushwa Mayahudi neema walizopewa, sio Utume unaendelea hata baada ya Uma huu au katika uma huu. Na haya tumeyabainisha mahala pengi; na pa kwanza katika Aya ya 7 ya *Al Fatiha*.

21. Hapa wanaambiwa waingie Falastini; na wanafanya ukaidi. Wala hawakuambiwa iwe yao daima. Wala Waislamu sio waliowatoa huko.

Warumi ndio waliowatoa maalafu ya miaka nyuma. Kisha Waislamu wakawatoa hao Warumi kiasi cha miaka alfeni leo. Vipi wanaambiwa Waislamu waliwatoa Mayahudi katika nchi yao? Nchi yao gani? Wao waliambiwa tu wakakae katika nchi hiyo ya Makan-ani; kisha wakatolewa na Warumi na waliokuwa kabla ya Warumi; khalafu Waislamu wakawatoa Warumi; wakasalia hapo kiasi cha miaka alfu mbili sasa. Vipi wanaambiwa si pao?

وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ ابْنَيْ اٰدَمَ بِالْحَقِّ ۘ اِذْ قَرَّبَا
قُرْبَانًا فَتُقُبِّلَ مِنْ اَحَدِهِمَا وَلَمْ يُتَقَبَّلْ
مِنَ الْاٰخَرِ ۭ قَالَ لَاَقْتُلَنَّكَ ۭ قَالَ اِنَّمَا يَتَقَبَّلُ
اللّٰهُ مِنَ الْمُتَّقِيْنَ ﴿٢٧﴾

27. Na wasomee khabari za watoto wawili wa Adamu kwa kweli. Walipotoa sadaka, ikakubaliwa ya mmoja wao, na ya mwengine haikukubaliwa. Akasema (yule isiyokubaliwa sadaka yake). "Nitakuua" Akasema (yule aliyehadidiwa kuuawa): "Mwenyezi Mungu huwapokelea wamchao tu."

لَىِٕنْۢ بَسَطْتَّ اِلَيَّ يَدَكَ لِتَقْتُلَنِيْ مَآ اَنَا بِبَاسِطٍ يَّدِيَ
اِلَيْكَ لِاَقْتُلَكَ ۚ اِنِّىْٓ اَخَافُ اللّٰهَ رَبَّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٢٨﴾

28. "Kama utanyosha mkono wako kwangu kuniua, mimi sitakunyoshea mkono wangu kukuua. Hakika mimi namwogopa Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu."

اِنِّىْٓ اُرِيْدُ اَنْ تَبُوْٓاَ بِاِثْمِيْ وَاِثْمِكَ فَتَكُوْنَ
مِنْ اَصْحٰبِ النَّارِ ۚ وَذٰلِكَ جَزٰۗؤُا الظّٰلِمِيْنَ ﴿٢٩﴾

29. "Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako; na kwa hivyo uwe miongoni mwa watu wa Motoni. Na hayo ndiyo malipo ya madhalimu."

فَطَوَّعَتْ لَهٗ نَفْسُهٗ قَتْلَ اَخِيْهِ فَقَتَلَهٗ فَاَصْبَحَ مِنَ
الْخٰسِرِيْنَ ﴿٣٠﴾

30. Basi nafsi yake ikamwezesha kumwua nduguye; akamwua: na akawa miongoni mwa wenye kukhasirika.

فَبَعَثَ اللّٰهُ غُرَابًا يَّبْحَثُ فِي الْاَرْضِ لِيُرِيَهٗ
كَيْفَ يُوَارِيْ سَوْءَةَ اَخِيْهِ ۭ قَالَ يٰوَيْلَتٰٓى اَعَجَزْتُ
اَنْ اَكُوْنَ مِثْلَ هٰذَا الْغُرَابِ فَاُوَارِيَ سَوْءَةَ
اَخِيْ ۭ فَاَصْبَحَ مِنَ النّٰدِمِيْنَ ﴿٣١﴾

31. Hapo Mwenyezi Mungu akamleta kunguru anayefukua katika ardhi ili amwonyeshe jinsi ya kuificha maiti ya ndugu yake. Akasema: (yule ndugu aliyeua): "Ole wangu! Nimeshindwa kuwa sawa na kunguru huyu na kuficha maiti ya ndugu yangu?" Basi akawa miongoni mwa wenye kujuta.

مِنْ اَجْلِ ذٰلِكَ ۚ كَتَبْنَا عَلٰي بَنِيْٓ اِسْرَاۗءِيْلَ اَنَّهٗ
مَنْ قَتَلَ نَفْسًۢا بِغَيْرِ نَفْسٍ اَوْ فَسَادٍ فِي
الْاَرْضِ فَكَاَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيْعًا ۭ وَمَنْ

32. Kwa sababu ya hayo tukawaandikia wana wa Israili ya kwamba atakayemwua mtu bila ya yeye kuua mtu, au bila ya kufanya fisadi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote; na mwenye kumwacha

---

Na Mayahudi wataitapika tu Falastini na nchi zote hizo walizozichukua na watakazozichukua kama watazichukua. Kuchukua huko ni kwa nguvu za madola makubwa yanayowasaidia. Ama wao wenyewe peke yao — maadamu hawatakuwa Waislamu — hawatakuwa na enzi kabisa. Ameyasema maneno haya Mwenyezi Mungu katika Qurani katika Aya ya 112 ya *Surat Aali Imran*.

Basi tusighurike na kushinda huku kwa Mayahudi; ni povu tu la . . . Litadidimia tu kama mapovu yote yanavyokuwa; ila mengine huchukua muda mrefu zaidi tu. Lakini kuondoka lazima.

26. Basi wakadumu kuhangaika majangwani bila kupumua; na huku ile mizee mikaidi inakufakufa; na chipukizi mpya zilizozaliwa humo jangwani zinanyanyuka kwa mwendo mzuri na utiifu. Basi baada ya miaka 40 chipukizi hawa ndio waliopigana na majabari wa Shamu, wakatawala wao.

27. Hiki ndicho kisa cha awali cha mtu kumwua mwenziwe.. Na huyu aliyeuawa ndiye binaadamu wa mwanzo kufa. Basi alidangana yule aliyeua, hajui amfanye nini — anazunguka naye tu mgongoni na anaogopa kurejea naye nyumbani aisijulikane na wazee wake. Na wazee wenyewe ni mwenyewe Nabii Adamu na Bibi Hawa. Na asijulikane na ndugu zao wengine.

Kwa bahati akatokea kunguru aliyepigana na mwenziwe akamwua, akamchimbia akamzika. Ndiyo na yeye akapata fikira ya kuzika.

N.B.—Binaadamu ndiye kiumbe cha mwisho kuja ulimwenguni. Ametanguliwa na viumbe vyote kwa myaka elfu nyingi kabisa. Namna hivi Qurani imesema zamani kabla ya kutambua hawa wanaosema sasa kwa jitihada za ilimu zao.

28. Aya hii haionyeshi kuwa mtu anakatazwa kujipigania. Naajipiganie ajitetee kwa kupigana mwenyewe au kupiga kelele kuweta wa kumsaidia. Ajipiganie nafasi yake, akipiganie chake, awapiganie wake, avipiganie vyao, awapiganie Waislamu wenzake, avipiganie vyao; bali awapiganie hata wasiokuwa Waislamu maadamu hawapigi, na

mtu hai (kumsaidia kuishi) ni kama amewaacha hai watu wote. Na bila shaka Mitume wetu waliwafikia na hoja zilizo wazi; kisha wengi katika wao baada ya haya walikuwa waharibifu sana katika nchi.

أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَآ أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا ۚ وَلَقَدْ
جَآءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَٰتِ ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُم
بَعْدَ ذَٰلِكَ فِى الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ ﴿٣٢﴾

33. Basi malipo ya wale wanaopigana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake (kwa kufanya aliyowakataza) na kufanya uovu katika nchi, ni kuuawa au kusulubiwa au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho; (mkono wa kulia kwa mguu wa kushoto, na mkono wa shoto kwa mguu wa kulia) au kuhamishwa katika nchi. Hii ndiyo fedheha yao katika dunia; na Akhera watapata adhabu kubwa.

إِنَّمَا جَزَٰٓؤُا۟ ٱلَّذِينَ يُحَارِبُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ
وَيَسْعَوْنَ فِى ٱلْأَرْضِ فَسَادًا أَن يُقَتَّلُوٓا۟
أَوْ يُصَلَّبُوٓا۟ أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُم مِّنْ
خِلَٰفٍ أَوْ يُنفَوْا۟ مِنَ ٱلْأَرْضِ ۚ ذَٰلِكَ لَهُمْ
خِزْىٌ فِى ٱلدُّنْيَا ۖ وَلَهُمْ فِى ٱلْءَاخِرَةِ عَذَابٌ
عَظِيمٌ ﴿٣٣﴾

34. Isipokuwa wale watakaotubia kabla hamjawakamata. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

إِلَّا ٱلَّذِينَ تَابُوا۟ مِن قَبْلِ أَن تَقْدِرُوا۟ عَلَيْهِمْ ۖ
فَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣٤﴾ ع ٩

35. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikilia (kufikilia Pepo Yake). Na piganeni kwa ajili ya dini Yake ili mpate kufaulu.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَٱبْتَغُوٓا۟ إِلَيْهِ
ٱلْوَسِيلَةَ وَجَٰهِدُوا۟ فِى سَبِيلِهِۦ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣٥﴾

---

avipiganie vyao maadamu si vya haramu. Bali avipiganie kila vyenye roho visifanyiwe lisilokubaliwa na Sharia. Na kwa yote haya anapata thawabu; kama zinavyoonyesha haya Aya za Qurani (kwa ufupi) na Hadithi za Mtume (kwa urefu).

Basi hivyo vyama vya Kuzuilia Ukatili kwa Wanyama vimefanywa na Waislamu zaidi ya myaka elfu mbele. Hawa Wazungu wanaiga tu. Waliona kwa Waislamu wakapenda, wakatamani kufanya, wakafanya.

Nda wenyewe mambo Wengine nda kutamani

Nayo ndio ndivyo; ukiona zuri uige. Usiseme: "Maadamu si Letu Hatulifuati." Ujinga huo sio Uislamu. Basi haya shime kuiga MAZURI siyo kuiga kinyani—ovyo tu; kuiga hata ya kudhuru. Tusiwe watu nyani au yatathibiti aliyoyasema Darwin. Na hali ya kuwa si kweli. Aya hii imesema: "Yeye hataanza kumpiga, siyo hatajipigania."

33. Hapa inatajwa adhabu ya kutiwa mafisadi wanaokatia watu njia — wanaojificha wakawashambulia watu. Basi watu hao:

(a) Ikiwa wanaua tu bila kuchukua mali ya hao wanaowaua. Basi wakipatikana hakimu ataamrisha wauawe tu.

(b) Ikiwa wanaua na kuchukua mali; basi hakimu ataamrisha wauawe; na baada ya kuuawa wasulubiwe muda wa siku tatu kabla ya kuzikwa; au ataamrisha wasulubiwe kwanza muda mfupi kiasi ya kutoka roho. Wakikurubia kutoka roho wateremshwe wauawe.

(c) Ikiwa hawaui lakini wananyang'anya mali tu; basi watakapokamatwa hakimu ataamrisha kila mmoja katika hao akatwe kiganja chake cha mkono wa kulia na unyayo wa kushoto AU kiganja cha kushoto na unyayo wa kulia.

(d) Ikiwa hawaui wala hawanyang'anyi, ila wanawataabisha tu watu na kuwatisha, basi hakimu ataamrisha watolewe nchi ile wakafungwe nchi ya mbali. Au wafungwe katika mji huo huo.

35. *Al Wasyla* ni jambo linalomfikisha mtu mahala fulani au linalomfikishia (linalompatia) kitu fulani. Na Mtume amekwisha kusema katika Hadithi zake sahihi kuwa hakuna la kumsogeza mtu likamfikisha katika radhi ya Mwenyezi Mungu kama kutekeleza aliyomwamrisha na kujiepusha na aliyoyakataza. Na moja ya hadithi hizi ni aliyotaja Imam al Bukhary kama ilivyo katika Hadithi ya 38 *Arbain* NAWAWY. Na kila Mwislamu anajua (a) yaliyokatazwa ni yapi (Imesalia kujiepusha nayo tu) na anajua (b) yaliyoamrishwa (Imesalia kuyafanya tu).

Basi haya natujiepushe na yaliyokatazwa yote kabisa na tufanye tuliyoamrishwa mwisho wa uweza wetu kabisa. Itakuwa tumekwisha kupata hii wasyla iliyotajwa hapa na katika Aya nyingine kama Aya ya 57 ya *Sura Bani*

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ أَنَّ لَهُم مَّا فِي الْأَرْضِ
جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ لِيَفْتَدُوا بِهِ مِنْ عَذَابِ يَوْمِ
الْقِيَامَةِ مَا تُقُبِّلَ مِنْهُمْ ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٣٦﴾
يُرِيدُونَ أَن يَخْرُجُوا مِنَ النَّارِ وَمَا هُم
بِخَارِجِينَ مِنْهَا ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٣٧﴾
وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا
جَزَاءً بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِّنَ اللَّهِ ۗ
وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٣٨﴾
فَمَن تَابَ مِن بَعْدِ ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللَّهَ
يَتُوبُ عَلَيْهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣٩﴾

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ
وَالْأَرْضِ ۖ يُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ وَيَغْفِرُ
لِمَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٠﴾

يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ لَا يَحْزُنكَ الَّذِينَ يُسَارِعُونَ فِي
الْكُفْرِ مِنَ الَّذِينَ قَالُوا آمَنَّا بِأَفْوَاهِهِمْ وَلَمْ
تُؤْمِن قُلُوبُهُمْ ۛ وَمِنَ الَّذِينَ هَادُوا ۛ
سَمَّاعُونَ لِلْكَذِبِ سَمَّاعُونَ لِقَوْمٍ آخَرِينَ ۙ
لَمْ يَأْتُوكَ ۚ يُحَرِّفُونَ الْكَلِمَ مِن بَعْدِ مَوَاضِعِهِ ۖ
يَقُولُونَ إِنْ أُوتِيتُمْ هَٰذَا فَخُذُوهُ وَإِن لَّمْ
تُؤْتَوْهُ فَاحْذَرُوا ۚ وَمَن يُرِدِ اللَّهُ فِتْنَتَهُ فَلَن

36. Kwa yakini, wale waliokufuru lau wangekuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya siku ya Kiyama, yasingalipokelewa kwao; na watapata adhabu iumizayo.

37. Watataka (kila namna) watoke katika Moto, lakini hawatatoka humo, na watakuwa na adhabu inayodumu (kwao).

38. Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao; malipo ya yale waliyoyachuma. Ndiyo adhabu, itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

39. Lakini mwenye kutubia baada ya dhulma yake, na akatenda wema, basi Mwenyezi Mungu atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

40. Je, hujui ya kwamba Mwenyezi Mungu anao ufalme wa mbingu na ardhi? Humwadhibu amtakaye (anapomkosa) na humsamehe amtakaye (anaporejea). Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

41. Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wale wafanyao haraka kukufuru, miongoni mwa wale wanaosema, kwa vinywa vyao, "Tumeamini," hali nyoyo zao haziamini; na miongoni mwa Mayahudi wanaokuja kusikiliza unayoyasema kwa ajili wakaseme uwongo; wanaokuja kusikiliza kwa ajili ya watu wengine wasiokufikia; (wale wakubwa wao ambao) huyabadilisha maneno (ya Taurati) baada ya kuwa mahali pake, ambao wanasema (kuwaambia hao wafuasi wao): "Mkipewa (na Muhammad) haya (tunayokwambieni) basi yashikeni, na msipopewa haya jihadharini." Na mtu ambaye Mwenyezi

---

Israili.

Siyo kusoma hiyo dua ISIYOFAA inayoitwa Wasyla ambayo ndani yake badala ya kumwomba Mwenyezi Mungu wanawaomba maiti wa Kisharifu waliozikwa Hadhramout. Baadhi ya yaliyomo humu ni haya:

"Wewe ndiye mwenyewe wa kutukidhia haja zetu. Basi twambie 'Ndiye Mimi.' Nani Mwenginewe wa kukukidhieni Haja zenu Nisiyekuwa Mimi."

Khalafu wanaendelea humo kwenye hiyo Wasyla yao kusema:

"Zimedhiki Haja zetu kila upande. Na Raj-wa zetu (tamaa) zimepiga magoti chini yako!"

Na mna humo mengi mno kabisa kama haya. Na kila mwaka wanazidisha vihendo vipya vipya utadhani wanawafanyia inda hao mashekhe wajuzi wanaowakataza. Wanamfanyia inda nani? Wanajidhuru wenyewe. Utadhani vijipaa vinavyopiga pembe jabali.

Mpiga konde ukuta Anajidhuru mwenyewe.

Tazama maelezo ya Aya ya 180 ya *Suratil Aaraf.*

38. Mwizi akiiba mara ya kwanza — kitu kikubwa — kitakatwa kiganja chake cha mkono wa kulia. Akiiba

تَمْلِكَ لَهٗ مِنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا ؕ اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ لَمْ
يُرِدِ اللّٰهُ اَنْ يُّطَهِّرَ قُلُوْبَهُمْ ؕ لَهُمْ فِى الدُّنْيَا
خِزْىٌ ۖ وَّلَهُمْ فِى الْاٰخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿٤١﴾

Mungu anataka kumtia mtihanini, huwezi kumpatia mbele ya Mwenyezi Mungu cho chote. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo zao (kwa kuwa wenyewe hawana raghba). Watakuwa na fedheha duniani; na katika Akhera watakuwa na adhabu kubwa.

سَمّٰعُوْنَ لِلْكَذِبِ اَكّٰلُوْنَ لِلسُّحْتِ ؕ فَاِنْ جَآءُوْكَ
فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ اَوْ اَعْرِضْ عَنْهُمْ ۚ وَاِنْ تُعْرِضْ
عَنْهُمْ فَلَنْ يَّضُرُّوْكَ شَيْـًٔا ؕ وَاِنْ حَكَمْتَ فَاحْكُمْ
بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِيْنَ ﴿٤٢﴾

42. Wasikiyao uwongo, walao haramu. Basi wakikujia, wahukumu baina yao au jipuze nao. Na ukijipuza nao, basi wao hawatakudhuru cho chote. Na ukiwahukumu, basi toa hukumu baina yao kwa uadilifu. Bila shaka Mwenyezi Mungu anawapenda waadilifu.

وَكَيْفَ يُحَكِّمُوْنَكَ وَعِنْدَهُمُ التَّوْرٰىةُ فِيْهَا
حُكْمُ اللّٰهِ ثُمَّ يَتَوَلَّوْنَ مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ ؕ وَمَآ اُولٰٓئِكَ
بِالْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٤٣﴾

43. Na watakuwekaje wewe kuwa hakimu, nao wanayo Taurati yenye hukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanakengeuka (unapowahukumu). Na hao si wenye kuamini (lo lote; basi tu wanafanya khadaa).

اِنَّآ اَنْزَلْنَا التَّوْرٰىةَ فِيْهَا هُدًى وَّنُوْرٌ ۚ يَحْكُمُ
بِهَا النَّبِيُّوْنَ الَّذِيْنَ اَسْلَمُوْا لِلَّذِيْنَ هَادُوْا
وَالرَّبّٰنِيُّوْنَ وَالْاَحْبَارُ بِمَا اسْتُحْفِظُوْا مِنْ كِتٰبِ
اللّٰهِ وَكَانُوْا عَلَيْهِ شُهَدَآءَ ۚ فَلَا تَخْشَوُا النَّاسَ
وَاخْشَوْنِ وَلَا تَشْتَرُوْا بِاٰيٰتِىْ ثَمَنًا قَلِيْلًا ؕ
وَمَنْ لَّمْ يَحْكُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ
الْكٰفِرُوْنَ ﴿٤٤﴾

44. Hakika tuliteremsha Taurati yenye uwongozi na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu; nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi (nyinyi Waislamu) msiwaogope watu, bali niogopeni (mimi). Wala msibadilishe Aya zangu kwa thamani chache (ya duniani). Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.

وَكَتَبْنَا عَلَيْهِمْ فِيْهَآ اَنَّ النَّفْسَ بِالنَّفْسِ ۙ
وَالْعَيْنَ بِالْعَيْنِ وَالْاَنْفَ بِالْاَنْفِ وَالْاُذُنَ
بِالْاُذُنِ وَالسِّنَّ بِالسِّنِّ ۙ وَالْجُرُوْحَ قِصَاصٌ ؕ

45. Na humo (katika Taurati) tuliwaandikia ya kwamba mtu (huuawa) kwa mtu, na jicho hutofolewa) kwa jicho, na pua (hukatwa kwa pua, na sikio (humeguliwa) kwa sikio, na jino (hung'olewa)

---

mara ya pili utakatwa unyayo wake wa mguu wa kushoto. Akiiba mara ya tatu kitakatwa kiganja cha mkono wake wa kushoto. Akiiba mara ya nne utakatwa unyayo wa mguu wake wa kulia. Akiiba mara ya tano ulamaa wengine wamesema kuwa hakimu ataamrisha auawe. Na wengine wamesema kuwa atatazamiwa hukumu nyengine yo yote lakini si kuuawa.

Hatujui kaifiya ya adhabu Mwenyezi Mungu atakayowapa makadiyani kwa kupoteza Waislamu. Wametaja katika Aya hii waliyoifanya kuwa ni ya 39 kuwa Sayyidna Ali amesema Vya kukatwa ni vidole, na kuwa maneno haya ameyataja na kuyakubali mwenye *Ruuhul Maany*. Na hali ya kuwa Mwenye *Ruuhul Maany* hakukubali kuwa Sayyidna Ali kasema hivi. Kayaweka wazi haya alipoifasiri Aya hii hapo katika hii Aya 38 ya *Suratul Maida* katika Juzuu ya Sita. Lakini basi tu wanataka kuwapoteza Waislamu.

39. Tazama rehema ya Mwenyezi Mungu anamuahidi asi kuwa akiacha mabaya yake atampokea — asijione kuwa amekwisha kuharibika, hatampokea.

41. Wanavyuoni wa Kiyahudi walikuwa wakiyageuza maneno ya Taurati na mahala pake, na wakigeuza tafsiri pia wanapowafundisha hao wafuasi wao. Kisha huwaambia 'Nendeni mkamsikilize mwongo huyo. Akisema kama hivi tunavyokwambieni basi ni kweli. Akisema vyengine jueni kuwa ni uwongo huo; na hali wanajua kuwa hawatosikia hayo wanayoyasema wao kwani hayo wanayoyasema wao ni uzushi waliouzuwa wao wenyewe. Na rejea Aya ya 15 ya hii hii *Suratul Maidah*.

kwa jino, na itakuwa kulipizwa kisasi katika kutiana majaraha. Lakini atakayesamehe basi itakuwa kafara kwake. Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu.

فَمَنْ تَصَدَّقَ بِهٖ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَّهٗ ؕ وَمَنْ لَّمْ يَحْكُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿٤٥﴾

46. Na Tukawafuatishia (Mitume hiyo) Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongozi na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na uwongozi na mauidha kwa wamchao (wanaomwogopa).

وَقَفَّيْنَا عَلٰٓى اٰثَارِهِمْ بِعِيْسَى ابْنِ مَرْيَمَ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرٰىةِ ۖ وَاٰتَيْنٰهُ الْاِنْجِيْلَ فِيْهِ هُدًى وَّنُوْرٌ ۙ وَّمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرٰىةِ وَهُدًى وَّمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِيْنَ ﴿٤٦﴾

47. Watu wa Injili wahukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu ndani yake. Na wasiohukumu kwa (kufuata) yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio maasi.

وَلْيَحْكُمْ اَهْلُ الْاِنْجِيْلِ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فِيْهِ ؕ وَمَنْ لَّمْ يَحْكُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿٤٧﴾

48. Na tumekuteremshia Kitabu kwa (ajili ya kubainisha) haki, kinachosadikisha vitabu vilivyokuwa kabla yake, na kuvihukumia (kama haya ndiyo yaliyoharibiwa au ndiyo yaliyosalimika). Basi wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki iliyokufikia. Na kila (uma) katika nyinyi (binaadamu) tumeujaalia sharia yake na njia yake. Na kama Mwenyezi Mungu angalitaka angekufanyeni kundi moja (la kufuata sharia moja), lakini anataka kukujaribuni kwa hayo aliyokupeni. Basi shindaneni kuyafikilia mambo ya kheri. Nyinyi nyote marudio yenu ni kwa Mwenyezi Mungu; naye atakwambieni (yote) yale mliyokuwa mkikhitilafiana.

وَاَنْزَلْنَآ اِلَيْكَ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتٰبِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ وَلَا تَتَّبِعْ اَهْوَآءَهُمْ عَمَّا جَآءَكَ مِنَ الْحَقِّ ؕ لِكُلٍّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَّمِنْهَاجًا ؕ وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ لَجَعَلَكُمْ اُمَّةً وَّاحِدَةً وَّلٰكِنْ لِّيَبْلُوَكُمْ فِيْ مَآ اٰتٰىكُمْ فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرٰتِ ؕ اِلَى اللّٰهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيْعًا فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيْهِ تَخْتَلِفُوْنَ ﴿٤٨﴾

49. Na wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao. Nawe jihadhari nao wasije kukugeuza na baadhi ya yale aliyokuteremshia

وَاَنِ احْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ وَلَا تَتَّبِعْ اَهْوَآءَهُمْ وَاحْذَرْهُمْ اَنْ يَّفْتِنُوْكَ عَنْ بَعْضِ مَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ اِلَيْكَ ؕ فَاِنْ تَوَلَّوْا فَاعْلَمْ اَنَّمَا

---

42. Wakati mwengine huja Mayahudi hao kwa Mtume ati awahukumu yeye katika kesi zao kwa kuwa yeye atawahukumu bila ya kupendelea — wala siyo madhumuni yao hayo. Basi anapewa khiari Mtume hapa kuwa akitaka awahukumu na akitaka anaweza kuwakatalia, kwani siyo makusudio yao kutaka la haki; wanataka wapate la takhfifu tu japokuwa silo.

44. Inasifiwa Taurati kitabu cha Nabii Musa kuwa kitabu hicho japokuwa aliteremshiwa Nabii Musa lakini Mitume wengi kabisa wa Kiyahudi waliokuja baada ya Nabii Musa waliambiwa wakifuate hiki hiki. Basi kikatumiwa na chungu ya Mitume na chungu ya wanavyuoni na chungu ya wacha Mungu. Na juu ya hivi chungu ya Mayahudi walikipinga, na mwisho wakakigeuzageuza watakavyo.

Makadiyani katika Aya hii walioifanya ya 45 wamepachika kwa undanindani ukafiri wao wa kumdaia Utume mtu wao. Lakini hawakuweza kujitokeza sana. Kila Mwislamu anajua kuwa anayejidaia kupewa Utume baada ya Nabii Muhammad ni kafiri. Na wanaomkubalia ni makafiri nao pia.

45. Zinatajwa baadhi ya hukumu zilizokuwamo humo.

46. Hapa inatajwa Injili—kitabu alichoteremshiwa Nabii Isa juu ya kuambiwa afuate na Taurati pia. Hii Injili ilikuwa ina mawaidha zaidi kuliko hukumu; na Taurati ina hukumu nyingi zaidi kuliko mawaidha. Ilivyokuwa

Mwenyezi Mungu. Na kama wakikengeuka, basi jua kwamba hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwafikishia (adhabu) kwa baadhi ya dhambi zao. Na bila shaka wengi katika watu ni maasi.

يُرِيْدُ اللّٰهُ اَنْ يُّصِيْبَهُمْ بِبَعْضِ ذُنُوْبِهِمْ ؕ وَ اِنَّ كَثِيْرًا مِّنَ النَّاسِ لَفٰسِقُوْنَ ﴿٤٩﴾

50. Je, wao wanataka hukumu za Kijahili (ya zile siku za ujinga kabla ya kuletwa Mtume)? Na nani aliye mwema zaidi katika hukumu kuliko Mwenyezi Mungu; (yanafahamika haya) kwa watu wenye yakini.

اَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُوْنَ ؕ وَمَنْ اَحْسَنُ مِنَ اللّٰهِ حُكْمًا لِّقَوْمٍ يُّوْقِنُوْنَ ﴿٥٠﴾

51. Enyi Mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa marafiki (wa kuwapa siri zenu); wao kwa wao ni marafiki. Na miongoni mwenu atakayefanya urafiki huo nao, basi huyo atakuwa pamoja nao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi (njia ya kheri) watu madhalimu.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُوْدَ وَ النَّصٰرٰۤى اَوْلِيَآءَ ۘ بَعْضُهُمْ اَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ؕ وَمَنْ يَّتَوَلَّهُمْ مِّنْكُمْ فَاِنَّهٗ مِنْهُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٥١﴾

52. Utawaona wale wenye ugonjwa nyoyoni mwao (nao ni wale wanafiki) wanakimbilia kwao (Mayahudi na makafiri wengine) wakisema: "Tunaogopa kutupata na sisi mgeuko (utakaowafika hawa Waislamu). Lakini karibu Mwenyezi Mungu ataleta kufungua miji au jambo (jingine) litokalo kwake, wawe wanafiki hawa ni) wenye majuto kwa yale waliyoyaficha katika nafsi zao.

فَتَرَى الَّذِيْنَ فِىْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ يُّسَارِعُوْنَ فِيْهِمْ يَقُوْلُوْنَ نَخْشٰۤى اَنْ تُصِيْبَنَا دَآئِرَةٌ ؕ فَعَسَى اللّٰهُ اَنْ يَّاْتِىَ بِالْفَتْحِ اَوْ اَمْرٍ مِّنْ عِنْدِهٖ فَيُصْبِحُوْا عَلٰى مَاۤ اَسَرُّوْا فِىْۤ اَنْفُسِهِمْ نٰدِمِيْنَ ﴿٥٢﴾

53. Na walioamini watasema (wakati huo watapofedheheka hao wanafiki): "Je, hao sio walioapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwa viapo vyao vigumu, ya kwamba wao wa pamoja nanyi? Vitendo vyao vimeharibika na wamekuwa wenye khasara."

وَيَقُوْلُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اَهٰۤؤُلَآءِ الَّذِيْنَ اَقْسَمُوْا بِاللّٰهِ جَهْدَ اَيْمَانِهِمْ ۙ اِنَّهُمْ لَمَعَكُمْ ؕ حَبِطَتْ اَعْمَالُهُمْ فَاَصْبَحُوْا خٰسِرِيْنَ ﴿٥٣﴾

54. Enyi mlioamini! Atakayeiacha miongoni mwenu dini yake, basi hivi karibuni Mwenyezi Mungu ataleta watu ambao atawapenda, nao watampenda, wanyenyekevu kwa Waislamu (wenzao), wenye nguvu juu ya makafiri.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مَنْ يَّرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنْ دِيْنِهٖ فَسَوْفَ يَاْتِى اللّٰهُ بِقَوْمٍ يُّحِبُّهُمْ وَيُحِبُّوْنَهٗۤ ۙ اَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ اَعِزَّةٍ عَلَى الْكٰفِرِيْنَ ۫ يُجَاهِدُوْنَ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَلَا يَخَافُوْنَ

---

mwishowe Mayahudi wameharibika sana ndiyo hiyo Injili ikajazwa mawaidha hivyo ili zilainike kidogo nyoyo za Mayahudi, lakini wapi.

Na huyu Nabii Isa alipelekwa kwa Mayahudi vile vile kama Nabii Musa, si kwa Wazungu; ila wengi kabisa walikataa kumfuata, akafuatwa na Wazungu kwa kulinganiwa na hao Mayahudi waliomfuata. Hawa Wazungu wamefuata nyuma, baada ya kuondoka ulimwenguni Nabii Isa kwani dini ya Mwenyezi Mungu haina wenyewe makhsusi.

48. Mitume wote wamekuja na hukumu moja katika Itikadi ya Mungu, Mitume, Malaika, Kiama, Tabia njema na kama haya.

Lakini katika mambo ya baadhi ya Hukumu wakikhitalifiana kidogo katika Sharia zao kwa mujibu wa nyakati zao hizo ambao ukikhitilafiana sana umbali wa nyakati wa baadhi ya Mitume na Mitume wengine, na mambo lazima yakhitalifu. Na kila anayoyafanya Mwenyezi Mungu, anayafanya kwa hikima.

49-50. Hapa wanahadidiwa wanaokataa hukumu alizotoa Mwenyezi Mungu, wakakhitari Mila ya Kienyeji *(Customary Laws na Decrees)*. Na wako watu namna hii. Basi wamo katika khatari kubwa kabisa. Juu ya kila Mwislamu kuridhia aliyoyasema Mwenyezi Mungu katika Qurani yake na aliyoyasema Mtume katika Hadithi zake SAHIHI. Akiyakataa haya basi kisha kusimama katika ukingo wa Moto wa Jahanamu tayari kutumbukia.

لَوْمَةَ لَآئِمٍ ۚ ذٰلِكَ فَضْلُ اللّٰهِ يُؤْتِيْهِ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَاللّٰهُ وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿٥٤﴾

Wataipigania dini ya Mwenyezi Mungu, wala hawataogopa lawama ya anayewalaumu. Hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa (na) Mwenye kujua.

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوا الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلٰوةَ وَيُؤْتُوْنَ الزَّكٰوةَ وَهُمْ رٰكِعُوْنَ ﴿٥٥﴾

55. Rafiki yenu khasa (wa kumsafia nia) ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini ambao husimamisha Sala na hutoa Zaka, na hali ya kuwa wananyenyekea.

وَمَنْ يَّتَوَلَّ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا فَاِنَّ حِزْبَ اللّٰهِ هُمُ الْغٰلِبُوْنَ ﴿٥٦﴾ ع

56. Na atakayefanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini (atafuzu) kwani (watu wa) kundi la Mwenyezi Mungu ndio watakaoshinda.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّخِذُوا الَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا دِيْنَكُمْ هُزُوًا وَّلَعِبًا مِّنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَالْكُفَّارَ اَوْلِيَآءَ ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٥٧﴾

57. Enyi mlioamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu miongoni mwa wale waliopewa kitabu kabla yenu na miongoni mwa makafiri (wengine). Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini.

وَاِذَا نَادَيْتُمْ اِلَى الصَّلٰوةِ اتَّخَذُوْهَا هُزُوًا وَّلَعِبًا ۚ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَعْقِلُوْنَ ﴿٥٨﴾

58. Na mnapoita kwendea Sala (mnapoadhini) wanaifanyia mzaha na mchezo. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.

قُلْ يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ هَلْ تَنْقِمُوْنَ مِنَّآ اِلَّآ اَنْ اٰمَنَّا بِاللّٰهِ وَمَآ اُنْزِلَ اِلَيْنَا وَمَآ اُنْزِلَ مِنْ قَبْلُ ۙ وَاَنَّ اَكْثَرَكُمْ فٰسِقُوْنَ ﴿٥٩﴾

59. Sema: "Enyi watu wa Kitabu! Je, mnatuona na kosa ila kuwa tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa na yale yaliyoteremshwa zamani, na kuwa wengi katika nyinyi ni maasi?" (Hatuna kosa jengine. Labda hili ndilo kosa letu kwenu).

قُلْ هَلْ اُنَبِّئُكُمْ بِشَرٍّ مِّنْ ذٰلِكَ مَثُوْبَةً عِنْدَ اللّٰهِ ۭ مَنْ لَّعَنَهُ اللّٰهُ وَغَضِبَ عَلَيْهِ وَجَعَلَ مِنْهُمُ الْقِرَدَةَ وَالْخَنَازِيْرَ وَعَبَدَ الطَّاغُوْتَ ۭ اُولٰۗىِٕكَ شَرٌّ مَّكَانًا وَّاَضَلُّ عَنْ سَوَاۗءِ السَّبِيْلِ ﴿٦٠﴾

60. Sema: "Je! Nikwambieni yule ambaye ni mwenye malipo mabaya zaidi kuliko haya mbele ya Mwenyezi Mungu? Ni ambao Mwenyezi Mungu amewalani na kuwakasirikia na kuwafanya wengine kuwa nyani na nguruwe, na wakamwabudu shetani. Hao ndio wenye mahali pabaya na wapotofu (wapotevu) sana (ambao wako mbali) na njia iliyo sawa."

---

51. Aya nyingi kabisa zimetukataza kuwafanya wasiri wetu; na baadhi yake tumekwisha kuzitaja. Tumehimizwa kuwafanyia (a) Uadilifu katika haki zao na (b) kuwafanyia mema kwa chetu na yetu. Ama kuwafanya wasiri wetu hapana ruhusa, kwani kila namna hawana usafi wa roho na sisi. Wana misiba ya nyoyo juu yetu na uadui wa milele.

52. Wanafiki walikuwa wakijitia huku (kwa Waislamu) na huko (kwa Makafiri), lakini mapenzi yao khasa ni kwa Makafiri lakini walikuwa wanafanya unafiki huo kwa kuogopa mabadiliko ya ulimwengu—wanaona wakitengenekewa hawa Makafiri watakuwa ni wenzao, na wakitengenekewa Waislamu watajifanya pia kuwa ni wenziwao kwani wakijidhihirisha mbele ya Waislamu kuwa ni Waislamu, wala si Waislamu, bali ni maadui wa Waislamu ila wanafanya unafiki tu.

54. Wanatiwa nguvu Waislamu kuwa wasivunjike nyoyo wakiona baadhi ya waliosilimu wanatoka Uislamuni, kwani Mwenyezi Mungu atawaleta mabora kuliko hao walioritadi, na ambao watakuwa na sifa za Uislamu khasa. Na akazitaja Mwenyezi Mungu katika hii Aya ya 54 na ya 55 na ya 56 baadhi ya sifa za Waislamu wa kweli. Basi natujitahidi tusifike nazo mwisho wa jitihada yetu.

وَ اِذَا جَآءُوْكُمْ قَالُوْٓا اٰمَنَّا وَقَدْ دَّخَلُوْا بِالْكُفْرِ وَهُمْ قَدْ خَرَجُوْا بِهٖ ؕ وَاللّٰهُ اَعْلَمُ بِمَا كَانُوْا يَكْتُمُوْنَ ﴿٦١﴾

61. Na (wanafiki) wanapokufikieni husema: "Tumeamini;" hali wao wameingia (kwenu hapo) pamoja na ukafiri (wao), na wao wametoka nao (ukafiri wao). Na Mwenyezi Mungu anayafahamu sana yote wanayoyaficha.

وَتَرٰى كَثِيْرًا مِّنْهُمْ يُسَارِعُوْنَ فِى الْاِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَاَكْلِهِمُ السُّحْتَ ؕ لَبِئْسَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٦٢﴾

62. Na utawaona wengi katika wao wanakimbilia katika dhambi na uadui na ulaji wao wa haramu. Bila shaka wayafanyayo hayo ni mabaya kabisa.

لَوْلَا يَنْهٰهُمُ الرَّبّٰنِيُّوْنَ وَالْاَحْبَارُ عَنْ قَوْلِهِمُ الْاِثْمَ وَاَكْلِهِمُ السُّحْتَ ؕ لَبِئْسَ مَا كَانُوْا يَصْنَعُوْنَ ﴿٦٣﴾

63. Mbona watawa (wao) na wanavyuoni wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi na ulaji wao wa haramu? Bila shaka wayatendayo ni mabaya kabisa.

وَقَالَتِ الْيَهُوْدُ يَدُ اللّٰهِ مَغْلُوْلَةٌ ؕ غُلَّتْ اَيْدِيْهِمْ وَلُعِنُوْا بِمَا قَالُوْا ۘ بَلْ يَدٰهُ مَبْسُوْطَتٰنِ ۙ يُنْفِقُ كَيْفَ يَشَآءُ ؕ وَلَيَزِيْدَنَّ كَثِيْرًا مِّنْهُمْ مَّآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ طُغْيَانًا وَّكُفْرًا ؕ وَاَلْقَيْنَا بَيْنَهُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَآءَ اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ ؕ كُلَّمَآ اَوْقَدُوْا نَارًا لِّلْحَرْبِ اَطْفَاَهَا اللّٰهُ ۙ وَيَسْعَوْنَ فِى الْاَرْضِ فَسَادًا ؕ وَاللّٰهُ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿٦٤﴾

64. Na Mayahudi walisema: "Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba; (hatuoni kupata mali kama zamani)." (Siyo, bali) mikono yao ndiyo iliyofumba (haifanyi kheri ila kudhulumu na kupokonya); na wamelaaniwa kwa sababu ya yale waliyosema. Lakini mikono yake (Mwenyezi Mungu) iwazi, hutoa apendavyo. Kwa yakini yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako yatawazidisha wengi katika wao (hao Mayahudi) uadui na kufuru. Na tumewatilia uadui na bughudha baina yao mpaka siku ya Kiyama. Kila mara wanapowasha moto wa vita Mwenyezi Mungu anauzima. Na wanajitahidi kuleta uharibifu katika ardhi (lakini Mwenyezi Mungu hasimami nao). Na Mwenyezi Mungu hawapendi waharibifu.

وَلَوْ اَنَّ اَهْلَ الْكِتٰبِ اٰمَنُوْا وَاتَّقَوْا لَكَفَّرْنَا عَنْهُمْ سَيِّاٰتِهِمْ وَلَاَدْخَلْنٰهُمْ جَنّٰتِ النَّعِيْمِ ﴿٦٥﴾

65. Na kama hawa watu wa Kitabu wangaliamini na kumcha Mwenyezi Mungu, bila shaka tungaliwafutia makosa yao na kuwaingiza katika Bustani zenye neema (kubwa kabisa).

وَلَوْ اَنَّهُمْ اَقَامُوا التَّوْرٰىةَ وَالْاِنْجِيْلَ وَمَآ اُنْزِلَ اِلَيْهِمْ مِّنْ رَّبِّهِمْ لَاَكَلُوْا مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ اَرْجُلِهِمْ ؕ مِنْهُمْ اُمَّةٌ مُّقْتَصِدَةٌ ؕ وَكَثِيْرٌ مِّنْهُمْ سَآءَ مَا يَعْمَلُوْنَ ﴿٦٦﴾

66. Na kama wangalisimamisha Taurati na Injili na yale yaliyoteremshwa kwao kutoka kwa Mola wao (Quran), kwa yakini wangalikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao. (Lakini) wako watu miongoni mwao washikao njia nzuri. (Lakini) wengi wao wanayoyafanya ni mabaya (kabisa).

---

57. Aya hii ni kama zile zile zilizopia zinazokataza kuwafanya wasiri wetu.

59. Wanatahayarishwa makafiri wanaowachukia Waislamu, wanaambiwa lipi baya lilofanyiwa na Waislamu? Kwani Waislamu wanakaa vizuri na kila mtu. Basi hawajaona baya lo lote walilofanyiwa na Waislamu. Lililowaudhi ni kule kufuata dini ya Kiislamu tu na kuwa wao—makafiri—ndio wabaya.

60. Wakubwa wa Kiyahudi wakiwadanganya wafuasi wao wakiwaambia ni 'Watu wabaya hawa wanaojita Waislamu na watakuwa na malipo mabaya.' Basi Mwenyezi Mungu anawabainishia kuwa wabaya ni wazee wao Mayahudi waliofanya mabaya yao hapo zamani hata Mwenyezi Mungu akawalani, akawakasirikia, akawageuza wengine kuwa manyama na kuwa wenye kuabudu dini zisizokuwa za haki.

يَاَيُّهَا الرَّسُوْلُ بَلِّغْ مَآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ ؕ
وَاِنْ لَّمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهٗ ؕ وَاللّٰهُ يَعْصِمُكَ
مِنَ النَّاسِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٦٧﴾

67. Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wanaokufuru.

قُلْ يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ لَسْتُمْ عَلٰى شَىْءٍ حَتّٰى تُقِيْمُوا
التَّوْرٰىةَ وَالْاِنْجِيْلَ وَمَآ اُنْزِلَ اِلَيْكُمْ مِّنْ رَّبِّكُمْ ؕ
وَلَيَزِيْدَنَّ كَثِيْرًا مِّنْهُمْ مَّآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ
طُغْيَانًا وَّكُفْرًا ۚ فَلَا تَاْسَ عَلَى الْقَوْمِ
الْكٰفِرِيْنَ ﴿٦٨﴾

68. Sema: "Enyi watu wa Kitabu! Hamko juu ya cho chote (katika dini yenu) mpaka msimamishe Taurati na Injili na haya yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu (Nayo ni Qurani)." Na bila shaka yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako yatawazidishia wengi katika wao uasi na kufuru. Basi usihuzunike kwa watu wanaokufuru.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَالَّذِيْنَ هَادُوْا وَالصّٰبِـُٔوْنَ
وَالنَّصٰرٰى مَنْ اٰمَنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَعَمِلَ
صَالِحًا فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٦٩﴾

69. Hakika wale walioamini (namna ya kikwao zamani) na Mayahudi na Masabii na Wakristo— watakaomwamini Mwenyezi Mungu (kama hivi anavyosema Nabii Muhammad) na siku ya mwisho na wakafanya vitendo vizuri basi hao hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika.

لَقَدْ اَخَذْنَا مِيْثَاقَ بَنِىْٓ اِسْرَآءِيْلَ وَاَرْسَلْنَآ
اِلَيْهِمْ رُسُلًا ؕ كُلَّمَا جَآءَهُمْ رَسُوْلٌۢ بِمَا لَا
تَهْوٰٓى اَنْفُسُهُمْ ۙ فَرِيْقًا كَذَّبُوْا وَفَرِيْقًا
يَّقْتُلُوْنَ ﴿٧٠﴾

70. Kwa yakini tulichukuwa ahadi ya wana wa Israili (Mayahudi kuwa watafuata), na tukawapelekea Mitume (Lakini) kila mara alipowafikia Mtume kwa yale zisiyoyapenda nafsi zao, wengine (katika Mitume hao) waliwakadhibisha, na wengine wakawaua (khasa).

وَحَسِبُوْٓا اَلَّا تَكُوْنَ فِتْنَةٌ فَعَمُوْا وَصَمُّوْا ثُمَّ
تَابَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ ثُمَّ عَمُوْا وَصَمُّوْا
كَثِيْرٌ مِّنْهُمْ ؕ وَاللّٰهُ بَصِيْرٌۢ بِمَا يَعْمَلُوْنَ ﴿٧١﴾

71. Na walidhani ya kwamba haitatokea adhabu, basi wakawa vipofu na viziwi, (wamo katika mabaya tu). Kisha Mwenyezi Mungu akawapokelea toba zao (walipotubia). Tena wengi katika wao wakawa vipofu na viziwi (tena). Na Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda.

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِيْنَ قَالُوْٓا اِنَّ اللّٰهَ هُوَ الْمَسِيْحُ
ابْنُ مَرْيَمَ ؕ

72. Bila ya shaka wamekufuru wale waliosema, "Mwenyezi Mungu ni Masihi (Isa) bin Maryamu."

Hapa pana tafsiri mbili. Makadiyani wameificha moja. Nayo ni kuwa Mayahudi hao maasi wakubwa waligeuzwa Manyani khasa na Makima khasa, kisha wakafa. Wao Makadiani, kwa ajili ya kukataa miujiza, wameificha tafsiri hii kusudi, na hali ya kuwa ndiyo yenye nguvu zaidi na ndiyo iliyofuatwa na Maimamu wengi zaidi kabisa, kama ilivyo katika sahifa 157 ya Juzuu ya 6 ya tafsiri ya *Ruuhul Maany* wanayojidai kuitaja mara kwa mara na kuwa wanaifuata. Waongo. Wao hamu yao ni kuharibu tu itikadi za Waislamu kwa kila kichochoro wanachoweza kukipata. Lakini Mwenyezi Mungu hatasimama nao.

64. Tunauona moto wa Kiyahudi unavyowaka na kuzimika mara kwa mara. Na mwisho utazimika kabisa fofofo. Mwenyezi Mungu kasema Mayahudi hawatapata ukubwa ulimwenguni ila kwa sharti mbili:

(a) Washikamane na mwendo mzuri aliouweka Mwenyezi Mungu; au

(b) Wawe wanapata msaada kwa dola nyenginezo; kama tunavyoona hivi.

Lakini wenyewe Mayahudi tu peke yao hawataweza kuwa chochote maisha yao. Tumetaja haya katika sura zilizopita. Ati wanamtia mori Mwenyezi azidi kuwapa kwa kusema "Siku hizi mkono wa Mwenyezi Mungu hautoi sana."

65-66. Wanatajiwa mambo ambayo lau wangeyafanya wangetengenekewa duniani na Akhera.

67. Anahimizwa hapa Mtume afikishe kila aliloambiwa, asibanie hata chembe wala asiogope lo lote kumfika.

وَقَالَ الْمَسِيحُ يٰبَنِيٓ إِسْرَآءِيلَ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۖ إِنَّهُ مَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَىٰهُ النَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّٰلِمِينَ مِنْ أَنصَارٍ ﴿٧٢﴾

Na (hali ya kuwa) Masihi alisema: "Enyi wana wa Israili! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu. Kwani anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahali pake (patakuwa) ni Motoni. Na madhalimu hawatakuwa na wasaidizi (wa kuwasaidia siku ya Kiama)."

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوٓا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَٰثَةٍ ۘ وَمَا مِنْ إِلَٰهٍ إِلَّآ إِلَٰهٌ وَٰحِدٌ ۚ وَإِن لَّمْ يَنتَهُوا عَمَّا يَقُولُونَ لَيَمَسَّنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٣﴾

73. Kwa hakika wamekufuru wale waliosema: "Mwenyezi Mungu ni mmoja katika (wale waungu) watatu; (yeye ndiye wa tatu wao)." Hali hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu mmoja (tu peke yake). Na kama hawataacha hayo wayasemayo, kwa yakini itawakamata—wale wanaoendelea na ukafiri miongoni mwao—adhabu iumizayo.

أَفَلَا يَتُوبُونَ إِلَى اللَّهِ وَيَسْتَغْفِرُونَهُ ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧٤﴾

74. Je! Hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na kumwomba msamaha? Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe na Mwingi wa Kurehemu.

مَّا الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ ۖ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ الرُّسُلُ ۖ وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ ۖ كَانَا يَأْكُلَانِ الطَّعَامَ ۗ انظُرْ كَيْفَ نُبَيِّنُ لَهُمُ الْآيَٰتِ ثُمَّ انظُرْ أَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ ﴿٧٥﴾

75. Masihi bin Maryamu si cho chote ila ni Mtume (tu). (Na) bila shaka Mitume wengi wamepita kabla yake. (Hawajaona)? Na mamake ni mwanamke mkweli. (Na) wote wawili walikuwa wakila chakula (na wakenda choo. Basi waungu gani wanaokula na kwenda choo)? Tazama jinsi tunavyowabainishia Aya, kisha tazama jinsi wanavyogeuzwa (kuacha haki).

قُلْ أَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا ۚ وَاللَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٧٦﴾

76. Sema: "Je! Mnawaabudu—badala ya Mwenyezi Mungu (peke yake)—wale ambao hawawezi kukudhuruni wala kukunufaisheni? Na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ndiye ajuaye.

قُلْ يٰٓأَهْلَ الْكِتَٰبِ لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ غَيْرَ الْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعُوٓا أَهْوَآءَ قَوْمٍ قَدْ ضَلُّوا مِن قَبْلُ وَأَضَلُّوا كَثِيرًا وَضَلُّوا عَن سَوَآءِ السَّبِيلِ ﴿٧٧﴾

77. Sema: "Enyi watu wa Kitabu! Msipindukie mipaka katika dini yenu bila haki, wala msifuate matamanio ya watu waliokwishapotea toka zamani; (nao ndio hao wanavyuoni wenu) na wakawapoteza wengi, na (sasa) wanapotea njia iliyo sawa, (hawataki kumfuata Nabii Muhammad).

Hakuna anayeweza kupitisha lake pasina Mwenyezi Mungu kutaka. Na kila wenye kujua wanaambiwa wabainishe vivi hivi — kinagaubaga — bila kuficha hata chembe wala kuogopa hata kidogo.

Wakikushituwa
Yupi awezaye
Wakiwa na lao

Wewe sishituke
Kupitisha lake
Mungu Ana Yake.

68,69. Anabainisha hapa Mwenyezi Mungu kuwa wenye dini zote—za Kiyahudi, za Kinasara, za Kisabai na nyinginezo—hawana salama ya Akhera ila kwa kufuata Uislamu (hiki Kitabu walichoteremshiwa sasa). Wakisha kufuata Uislamu wamekwisha kusalimika. Wala wasiseme: 'Hatutakubaliwa maadamu tulikuwa katika dini hizo zilizoharibiwa.' Hapana haya. Watakubaliwa tu na Bwana wao Mwenyezi Mungu kama Mwenyewe Alivyotoa

لُعِنَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ عَلٰى لِسَانِ دَاوٗدَ وَعِيْسَى ابْنِ مَرْيَمَ ؕ ذٰلِكَ بِمَا عَصَوْا وَّكَانُوْا يَعْتَدُوْنَ ۝٧٨

78. Walilaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israili kwa ulimi wa Daudi na wa Isa bin Maryamu. Hayo ni kwa sababu waliasi na wakipindukia mipaka (sana).

كَانُوْا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَنْ مُّنْكَرٍ فَعَلُوْهُ ؕ لَبِئْسَ مَا كَانُوْا يَفْعَلُوْنَ ۝٧٩

79. Hawakuwa wenye kuzuiana (kukatazana) mambo mabaya waliyokuwa wakiyafanya. Uovu ulioje wa jambo hili walilokuwa wakilifanya.

تَرٰى كَثِيْرًا مِّنْهُمْ يَتَوَلَّوْنَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ؕ لَبِئْسَ مَا قَدَّمَتْ لَهُمْ اَنْفُسُهُمْ اَنْ سَخِطَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ وَفِي الْعَذَابِ هُمْ خٰلِدُوْنَ ۝٨٠

80. Utawaona wengi katika wao (Mayahudi) wanafanya urafiki na waliokufuru (makafiri wa Kiarabu ili waipinge dini ya Uislamu, na hali ya kuwa hawa Mayahudi wanajua kuwa ni dini ya haki). Mabaya kabisa haya waliyotanguliziwa na nafsi zao. Nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu amewakasirikia, nao watakaa milele katika adhabu.

وَلَوْ كَانُوْا يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالنَّبِيِّ وَمَآ اُنْزِلَ اِلَيْهِ مَا اتَّخَذُوْهُمْ اَوْلِيَآءَ وَلٰكِنَّ كَثِيْرًا مِّنْهُمْ فٰسِقُوْنَ ۝٨١

81. Na lau wangalimwamini Mwenyezi Mungu (vilivyo) na (huyu) Nabii (Muhammad) na yaliyoteremshwa kwake, wasingaliwafanya hao kuwa marafiki (kwani hao ni maadui wa dini). Lakini wengi katika wao ni maasi.

لَتَجِدَنَّ اَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوا الْيَهُوْدَ وَالَّذِيْنَ اَشْرَكُوْا ۚ وَلَتَجِدَنَّ اَقْرَبَهُمْ مَّوَدَّةً لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوا الَّذِيْنَ قَالُوْٓا اِنَّا نَصٰرٰى ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّ مِنْهُمْ قِسِّيْسِيْنَ وَرُهْبَانًا وَّاَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُوْنَ ۝٨٢

82. Hakika utawakuta walio maadui zaidi kuliko watu (wengine) kwa Waislamu ni Mayahudi na wale mushirikina (wasiokuwa na Kitabu), na utawaona walio karibu kwa urafiki na Waislamu ni wale wanaosema: "Sisi ni Wakristo." (Hayo) ni kwa sababu wako miongoni mwao wanavyuoni na wachao Mungu, na kwa sababu wao (Wakristo) hawatakabari; (wakiijua haki huifuata).

---

ahadi, akasema katika Aya ya 38 ya *Suratul Anfal*. Na watapata watakayoyapata wema wengine. Lakini wakikakamia katika dini zao hizo—na hali ya kuwa wanajua kuwa za batili—basi hautakabaliwi kwao wema wo wote wanaoufanya.

71. Unatajwa uovu wa Mayahudi, kujidai kutubu, kisha wakayarejea yale yale.

72-73. Unatajwa ukafiri wa Kinasara kwa Itikadi zao zote tatu kuwa Nabii Isa (a) Mungu au (b) Mtoto wa Mungu au (c) Mmoja katika hao waungu watatu.

Yoyote katika itikadi hizi ni ukafiri usiokuwa na shaka, na jaza yake ni Moto tu.

74. Wanatiwa moyo makafiri kuwa wakiwacha ukafiri wao wo wote ule Mwenyezi Mungu atawapokea tu kama tulivyosema katika Aya 68 na 69 za sura hii.

75-76. Wanaonyeshwa kuwa Nabii Isa kama Mitume wengine, si Mungu. Kuna Mungu anayeshikwa na njaa akala, na kisha akabanwa na choo ikambidi kwenda kutoa hicho choo akitaka asitake? Basi si Mungu Nabii Isa, yeye kama Mitume wengine. Na ikiwa hakuzaliwa na baba, basi Nabii Adamu hakuzaliwa na baba wala mama pia. Basi yeye atastahiki uungu zaidi ikiwa hii ndiyo sababu.

Na wanabainishiwa kuwa Nabii Isa ni kama Mitume wengine, hamiliki kudhuru wala kunufaisha. Mambo yote yamo katika Mikono ya Mwenyezi Mungu wa haki.

Mambo yote ni ya Mungu
Ndiye Pweke Mwenye quwa

Atakalo ndilo huwa
Mwenye Amri na shani

77. Hapa wanakatazwa hao (a) Mayahudi kupindukia mipaka kwao hata wakamfanya Uzayri kuwa ni mtoto